
SportPesa
TZS. 896,686,220
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wanane** upinzani kuchuana na Tulia Uspika

UKURASA 4



**GREENWOOD AKAMATWA KWA TUHUMA ZA UBAKAJI**

UKURASA 21

Nipashe
Jumanne Februari 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580843
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
r.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Maumivu mgawo saa 16 bila umeme

• **Maeneo** ambayo hayataathirika yatajwa, bosi TANESCO afunguka... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**SABAYA ATAJWA KESI YA MBOWE**
LUTENI Dennis Urio amedai mahakamani kwamba katika ushahidi wake hakumtaja aliyekuwa Mkuu wa Wilaya...

UKURASA WA 19
**MAPIGANO WAKULIMA NA WAFUGAJI YAUA 6**
WATU sita wameuawa katika mapigano ya wakulima na wafugaji kwenye vijiji viwili mikoa ya Tanga...

UKURASA WA 19
**KAMATI YAUNDWA KUDHIBITI MAUAJI**
SERIKALI imeunda kamati itakayokuja na mkakati wa kitaifa utakaotoa suluhu ya kudumu ya kudhibiti matukio ya...

**Chaneli za ndani sasa kupatikana king'amuzi cha DSTv**

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisisitiza jambo wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo vya habari, waandishi wa magazeti na TV (hawapo pichani), uliofanyika ukumbi wa Ikulu jijini Zanzibar, jana. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi aahidi mabadiliko kwenye serikali yake

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA SC SASA MGUU SAWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba (kushoto), akizungumza katika mkutano na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CITI anayesimamia nchi za Afrika-Kusini mwa Jangwa la Sahara, Akinsowon Dawodu, uliohusu upatikanaji wa mikopo nafuu kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo nchini jijini Dodoma jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Maumivu mgawo saa 16 bila kuwa na umeme

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limetoa ratiba ya mgawo wa umeme utakaoanza leo hadi Februari 10, mwaka huu, ambapo mikoa 19 imetajwa huku nishati hiyo ikikosekana kwa saa 16 kwa siku.

Ratiba hiyo iliyotolewa jana, inaonyesha kuwa mikoa 12 haitaathiriwa na mgawo huo, ambao utakuwa ukianza saa 02:00 asubuhi hadi 6:00 usiku.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano TANESCO, maeneo ya hospitali na jeshi hayataathirika.

Mikoa ambayo haitaathirika kwa mgawo ni Bukoba, Katavi, Kigoma, Lindi, Mtwara, Pemba Kaskazini na Kusini, Rukwa, Simiyu, Zanzibar, Unguja Kaskazini na Magharibi.

Pia ilibainisha mikoa itakayoathirika ni Dar es Salaam (Temeke, Kinondoni na Ilala), Kilimanjaro na wilaya zake, Arusha, Mara, Mbeya, Manyara, Njombe, Morogoro, Mwanza, Singida, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Tanga, Tabora, Dodoma, Songwe, Iringa na Geita.

**KAULI YA MKURUGENZI**

Jana Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alitembelea kituo cha kupozea umeme cha Kunduchi mkoani Dar es Salaam na kutoa ufafanuzi kuhusiana na suala la kukatika kwa umeme katika maeneo yaliyoorodhesha, akisema kwamba hakuna eneo umeme utakatika kwa siku tatu mfululizo.

"Tunaendelea na maboresho kama tulivyosema tunajipanga, na kujipanga ni kujua matatizo, kujua majawabu yake na kuwa na mipango ya kuitatua," alisema na kuendelea:

"Tanzania nzima tunajua kila mahali tatizo ni nini, majawabu ni nini na tarehe ya kuyatatua ni lini, kwa hiyo kwa sasa tupo kazini kutekeleza."

Aliongeza kuwa katika zoezi la kuongeza mitambo ya uzalishaji wa umeme, kutakuwa na uhitaji wa gesi zaidi, akifafanua kuwa hilo linalazimu maboresho kufanyika katika visima vya gesi.

Alisema wakati maboresho hayo yanafanyika, watatumia siku 10 kufanya uboreshaji wa miundombinu ya umeme, huku akieleza kuwa hilo litasababisha umeme kukatwa kwa baadhi ya maeneo na siyo nchi nzima kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakisema.

"Tumeona kwamba watu wanataka ufafanuzi, kwani baadhi wanasema nchi itakuwa gizani, sasa nchi ikiwa gizani ni kwamba hatuonani humu jambo ambalo si kweli, ni sawa na chumbani kwako balbu moja ikiungua huwezi kusema nyumba iko gizani," alisema Chande.

"Ukweli ni kwamba kutakuwa na mapungufu, kuna maeneo hayatakuwa na umeme ratiba tumeshaitoa, lakini yatakayokuwa na umeme ni mengi... hii kazi tunayoifanya ni ya muhimu na faida kwa wote, hivyo ukisema nchi iko gizani inaweza kuleta taharuki," alisema Chande.

"Sisi tulitoa hii taarifa kwa sababu tuna wajibu wa kuwaambia wateja wetu nini kinatokea, lakini tungeweza pia kunyamaza tu halafu ikitokea siku hiyo hakuna umeme tutakupa hadithi nyingine, lakini huyo si weledi, weledi ni kuwaeleza, na wananchi wanaelewa na wanashirikiana nasi kuhakikisha tunaboresha," aliongeza Chande.

Alibainisha kuwa upungufu wa umeme utakaojitokeza hautasababishwa na maboresho wanayoyafanya, ila yatatokana na maboresho yanayofanyika katika visima vya gesi, ambayo hutumika katika uzalishaji, hivyo alisema kuwa watatumia muda huo kufanya maboresho ya miundombinu ya nishati hiyo sambamba na kuifikisha maeneo ambayo haijafika.

Pia alisema kuwa jumla ya upungufu wa umeme haizidi asilimia 25 ya uzalishaji wao wote, hivyo kusaidia sehemu kubwa kuendelea kubaki na umeme, na kuahidi kuwa wataendelea kupanga ratiba ili kusaidia maeneo husika kutoathirika kwa muda wote.

## Chaneli za ndani sasa kupatikana king'amuzi cha DSTV

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ametangaza kurejeshwa kwa chaneli za ndani kwenye mfumo wa matangazo wa moja kwa moja wa Satelite (DTH) kuanzia wiki hii.

Aliyasema hayo jana alipotembelea ofisi za kampuni ya MultiChoice Tanzania (DStv) ikiwa ni sehemu ya ziara zake kwa wadau wa wizara anayoingoza.

Waziri Nape alisema serikali imefanya mapitio ya kanuni za sekta ya utangazaji nchini na kwa mujibu wa marekebisho hayo sasa visimbuzi vyote vya antena (DTT) vile vya dish (DTH) vitaruhusiwa kubeba chaneli hizo.

Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya habari popote waliko bila usumbufu na kwa njia wanayoipendelea wao wenyewe.

"Tumefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya habari na tumefanikiwa kufanya marekebisho kwenye kanuni kadhaa na lengo la haya yote ni kuhakikisha kuwa Mtanzania popote aliko anapata habari, elimu na burudani kupitia mifumo na mitandao mbalimbali bila vikwazo," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, alimpongeza waziri na wizara kwa ujumla kwa kukamilisha mapitio ya kanuni mbalimbali za sekta ya utangazaji zilizoruhusu kuonyeshwa kwa chaneli za ndani kwenye mifumo mingi zaidi.

"Tumefurahishwa na mabadiliko haya ambayo kimsingi yanajibu mahitaji ya wananchi wetu wengi ambao kila uchao walikuwa wakiomba kuruhusiwa kwa chaneli za ndani katika visimbuzi vya DStv na vingine.

Tunaamini hii ni hatua muhimu kwa kuwa itawarahisishia zaidi wananchi kupata huduma za matangazo kwa urahisi," alisema Jacqueline.

Mkurugenzi huyo alisema DStv itatekeleza agizo la waziri kwa kuhakikisha kuwa wanaharakisha mchakato wa kuzibeba chaneli hizo ndani ya muda mfupi.

"Tumesikia maagizo ya waziri na mara moja tumeanza mazungumzo na chaneli husika ili tuweze kuzibeba ndani ya DStv na hivi karibuni.

Kurejea kwa chaneli hizo kutakifanya kisimbuzi hicho kuwa na zaidi ya chaneli zaidi ya 160 za ndani na nje ya nchi zikiwamo za michezo na burudani, habari na matukio, makala, elimu na za watoto.

Mapema mwaka 2018 chaneli za ndani ziliondolewa kwenye visimbuzi vya dishi kitendo kilichosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwani wengi walishindwa kuzipata chaneli hizo kama ITV, EATV, Clouds TV, Channel Ten, Star TV na hata chaneli za dini kama vile Imaan TV, Upendo TV na nyinginezo.

Baada ya DSTV kuweka taarifa hiyo ya waziri kwenye mitandao ya kijamii watumiaji wa king'amuzi hicho walionekana kuifurahia.

Katika ukurasa wa Instagram mtumiaji mwenye ishekibobo aliandika: "Ahsante sana mama Samia na Waziri Nape wamerejesha chaneli za bure, DSTV nao wafanye maboresho kwenye zao".

Wakati mtumiaje mwenye jina officialcau_tz aliandika "Nashukuru sana kwa hili@nappe_nnauye, nakukubali sana.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi aahidi mabadiliko serikali yake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ataendelea kufanya mabadiliko ya uongozi katika serikali yake kutokana na kutoridhishwa na uwajibikaji wa baadhi ya viongozi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Mjini hapo, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika utaratibu wake aliouweka wa kuzungumza nao kila mwisho wa mwezi.

Alisema utendaji serikalini una mafanikio na changamoto na kukiri kuwa bado katika serikali anayoiongoza zipo changamoto ikiwamo baadhi ya watendaji kutowajibika.

"Katika wateuliwa wapo wanaofanya vizuri na wapo ambao hawafanyi vizuri na hao ambao hawafanyi vizuri nitachukua hatua za kufanya mabadiliko, hili wala si siri," alisema.

Alisema kuwa mabadiliko hayo hayatohusisha Baraza la Mawaziri pekee bali hata mfanyakazi wa serikali asiye wajibika, hatabaki sehemu aliyoko mpaka astaafu ajiandae kuondolewa.

Dk. Mwinyi ameendelea kuwaunga mkono wanawake katika nafasi za uongozi na kusifu kuwa kati ya viongozi aliowateua wanawake ndiyo wanaofanya vizuri zaidi kuliko wanaume.

Tangu Rais Mwinyi alipounda baraza lake la mawaziri Novemba mwaka 2020, hajafanya mabadiliko na kuahidi kuyafanya hivi karibuni ili kuongeza ufanisi wa kazi.

"Yule ambaye anafanya vizuri nitaendelea naye na yule ambaye hafanyi vizuri atatupisha namuweka pembeni," alisema Dk. Mwinyi kwa kusisitiza mara kwa mara.

Vile vile, Dk. Mwinyi alisema amepokea ushauri wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuigawa Wizara ya Afya na atafanya kazi hiyo hiyo ili iwe inajitegemea.

Alisema kazi hiyo ataifanya hivi karibu ili kuwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu hatua hiyo ya rais kufanya mabadiliko ya uongozi katika serikali yake, baadhi ya wananchi walisema ni hatua nzuri na wale ambao hawaendani na kasi yake ya utendaji ni vyema akawaweka pembeni.

"Tunasubiri kwa hamu mabadiliko atakayoyafanya Rais hasa katika baraza lake la mawaziri kwa sababu baadhi ya mawaziri wake hawaendi na kasi yake ya ufanyaji kazi," alisema Juma Khamis, mfanyabiashara katika eneo la Mchangani Mjini Zanzibar.

Ali Issa Makame, mwanaharakati wa haki za binadamu, alisema kuwa marais wengi ambao wanakaa madarakani huwa hawadumu na baraza moja la mawaziri wote mpaka amalize uongozi wake, kwa sababu wengine anaowateua uwezo wao hauwezi kuonekana mpaka aingie katika utendaji.

Alisema kuwa katika kipindi cha uongozi cha mwaka mmoja wa Dk. Mwinyi kuna baadhi ya wizara zinahitaji kufanyiwa mabadiliko kutoka kwa makatibu wakuu, waziri na wakurugenzi hivyo mabadiliko hayo wananchi wanayasubiri kwa hamu.

"Wananchi wanaamini kuwa anachokisema Rais Dk. Mwinyi huwa anakitekeleza hivyo wanasubiri utekelezaji wake na kufanya mabadiliko hayo ili kupatata watendaji wanaoendana na kasi yake," alisema.

Alisema kuwa asilimia 90 ya watendaji ambao anao katika baraza la mawaziri ni wapya na katika mabadiliko yake anayotarajia kuyafanya anaweza kuchanganya wa zamani na wapya ili malengo aliyoyapanga katika uchumi wa buluu yafanikiwe kwa sababu baadhi ya wizara hazijawa na ubunifu wa utendaji.

Naye Yussuf Mchenga mkazi wa Mjini Unguja, alisema mabadiliko ya baraza la mawaziri ni sawa na timu ya mpira pale ambapo wachezaji hawafanyi vizuri kiongozi mkuu anahaki ya kubadilisha ili kupata maendeleo.

"Suala la mabadiliko la mawaziri ni la kawaida na wananchi wanahitaji maendeleo na ili maendeleo yapatikane lazima kuwapo na mabadiliko hivyo mimi namuunga mkono kwa hili," alisema.

## ...Asikitishwa wanaohujumu miundombinu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesikitishwa na vitendo vya wizi alivyoviita ni uhujumu wa uchumi wa kuiba nyanya katika visima vya kusambaza maji na kusababisha kutofanya kazi na wananchi kukosa maji.

Alisema tukio hilo limefanyika juzi katika visima vya maji huko Bubwisudi na tukio ambalo limefanyika mwaka jana la kuiba nyaya za shaba katika taa zote za barabarani eneo la daraja bovu Mjini Unguja.

Alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuwasaka wahalifu wa matukio hayo na watakapopatikana washtakiwe kwa kosa la uhujumu uchumi kwa sababu wamesababisha mji kuwa giza na wananchi kukosa maji.

"Natoa agizo kwa vyombo vya ulinzi na usalama hasa vikosi vya SMZ kuhakikisha maeneo haya nyeti ya maji na umeme yanalindwa badala ya ulinzi wa kawaida ili yasiendelee kuhujumiwa," alisema.

Alisema ifike muda wa kupiga marufuku biashara ya vyuma chakavu ili kuinusuru miundombinu na uharibifu huo.

Akizungumzia miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa masoko, alisema serikali ilitoa ahadi ya maeneo hayo kuyajenga upya ili kuwa na mejengo ya kisasa na tayari yameanza ujenzi huo ikiwamo eneo la Darajani, Soko la Mwanakwerekwe, Soko la Jumbi na Soko la Chuini.

Alisema wapo wananchi wameanza kupata taharuki katika ujenzi wa maeneo hayo kwa kuhofia kuondolewa na hawatozingatiwa wakati wa ujenzi utakapokamilika.

"Niwatoe hofu lengo la serikali ni kutengeneza mazingira mazuri kwa wajasiriamali wetu ili kufanya kazi katika mazingira mazuri hivyo wote waliopisha ujenzi katika maeneo hayo watapewa kipaumbele cha kwanza kabla ya wengine ambao hawapo katika maeneo hayo," alisema.

Akizungumzia ziara yake ya hivi karibu katika nchi za Falme za Kiarabu, alisema katika ziara hiyo amepata nafasi ya kuweka mkataba wa ujenzi wa eneo la Kizingo, lengo ni kulijenga eneo hilo ili kuwa taswira nzuri ya nchi na wavuvi na vijana wanaotumia eneo hilo kunufaika ikiwamo kujengewa soko la samaki la kisasa.

Kuhusu mji mkongwe wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, alisema ni urithi wa dunia lazima ulindwe na una zaidi ya miaka 100 ili vizazi vijavyo kuujua hivyo ni lazima majengo yake yaliochakaa na kubomoka kufanyiwa matengenezo.

Alisema nyumba nyingi katika mji huo hazipo katika hali nzuri na haziwezi kufika miaka mngine 100 ya baadaye na kwamba serikali imeamua wawekezaji au wananchi wenye uwezo kuzitengeneza.

"Serikali haina nia ya kumwondoa mtu katika nyumba hizo bali zifanyiwe matengenezo ili zisiendelee kuanguka kama ilivyo sasa."

Kuhusu fedha za UVIKO-19 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Sh. bilioni 230, alisema kuwa zitatumika kwa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa hospitali na shule na tayari miradi hiyo imeanza kujengwa.

Alisema nia na madhumuni ni kuwa na madarasa mingi ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, kuwa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia na elimu ya Zanzibar kubadilika.

Dk. Mwinyi aliwataka makandarasi wote waliopewa kazi hiyo kuhakikisha wanamaliza kwa muda uliotakiwa na serikali itatoa fedha bila ya kikwazo chochote ili kutokuwa na uzembe katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Pia alisema serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuufanya ukarabati Uwanja wa Ndege wa Pemba ili uweze kufanana na wa Unguja na ndege kubwa kutua ili uchumi upande.


COSMOS PROPERTIES

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Cosmos Properties Limited tumeona taarifa potofu kwenye vyombo vya habari ambazo zinazidi kusambaa kwenye mitandao ya kijamii zikiashiria kuwa jengo la uhuru height limeuzwa na kwamba kampuni yetu inakwenda kufilisika. Tunapenda kuutaarifu umma kuwa taarifa zinazosambaa kwenye vyombo vya habari mbalimbali kwa njia tofauti siyo za kweli na zinalengo la kuharibu taswira nzuri ya kibiashara ambayo kampuni ya Cosmos Properties Limited imeitengeneza kwa muda mrefu.

Kitu ambacho tumejidhatiti kuendelea kuilinda taswira yetu halali na biashara yetu kwa ujumla. Kwa ajili ya kuweka rekodi zetu sawa napenda kuwajulisha umma yafuatayo:-

1. Kampuni yetu inamahusiano ya kibiashara ya benki ya Exim Tanzania kama benki yetu na mkopeshaji wa rasilirimali fedha dhidi ya mali ambazo Uhuru Height waliziweka kama dhamana\ amana.
2. Kampuni yetu pamoja na Exim benki Tanzania Limited tunakesi namba 176\2021 ambayo inaendelea Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam
3. Pia tumepokea zuio la mahakama dhidi ya Exim benk Tanzani, wafanyakazi wake au mawakala wake hawatoruhusiwa kusaini, kutupa au kuhamisha mali zozote zilizoshtakiwa zilizopo Uhuru Height.
4. Kwa kushangaza na bila kutarajia mnamo tarehe 26 Januari 2022 tuliona magazeti na vyombo vya habari kuwa Exim benki wamemchagua Walter Buxton Chipeta kama Mfilisi wao na Meneja kuhusiana mali zote za Uhuru Height , Hili limefanyika muda ambao Exim wanaelewa ama wanafahamu kuhusu zuio la mahakama na Mr Chipeta kutoka kampuni ya uwakili ya Hallmark ni mwakilishi wa Exim benki katika shauri linaloendelea 176\2021.
5. Katika maendeleo mengine yasiyotarajiwa siku hiyo hiyo ya tarehe 26 Januari 2022 Mr. Chipeta alivamia Uhuru Height akiambatana na watu Zaidi ya 20 wasiofahamika ,, watu anaodai kuwa ni usalama wake binafsi .Hatukuwa na miadi yoyote ya nyuma na Mr Chipeta na hatukujihusisha kwenye jambo lolote kwa sababu ya zuio la Mahakama.
6. Tumeisha ripoti uvamizi huo kwenye mamlaka husika na tutachukua hatua stahiki za kisheria kulinda mali zetu na kuhakikisha kuwa utaratibu wa kimahakama unaheshimiwa kwa ujumla.
7. Kama unavyoona kwenye taarifa hii mali zilizopo Uhuru Height hazijauzwa na kampuni yetu haijafilisiliwa.

MKURUGENZI MKUU WA COSMOS PROPERTIES LIMITED
MUHAMMAD OWAIS PARDESI

COSMOS PROPERTIES LIMITED · DAR ES SALAAM · P.O. Box 2205

Cosmos Properties Ltd : Plot # 63/27,3rd Floor. Uhuru Heights, Bibi Titi Road, Upanga
P.O Box 2205 Dar es Salaam - Tanzania, Tel # +255 22 215 3317 / +255 22 215 1496
info@cosmosgrp.com / www.cosmosgrp.com



Askari wa Jiji wakichoma moto meza za wafanyabiashara wadogo maarufu machinga kuhakikisha hawarejei katika eneo la Mbezi Mwisho, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## KESI YA MBOWE

# Shahidi: Sikumtaja Sabaya angedhuriwa

**Na Kulwa Mzee**

LUTENI Dennis Urio amedai mahakamani kwamba katika ushahidi wake hakumtaja aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya kwamba washtakiwa wanapanga kumdhuru bali alisema viongozi.

Amedai Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alimwomba amtafutie watu wa kufanya ulinzi si magaidi, shahidi amekiri kwamba maelezo aliyotoa polisi na anachosema kwenye kizimba vinatofautiana.

Shahidi huyo wa 12 wa upande wa mashtaka katika kesi ya ugaidi inayomkabili, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala.

Luteni Urio anadai hafahamu kwanini alichukuliwa maelezo Agosti 11 mwaka 2020 na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), hakumfafanulia kwanini maelezo yake hayajachukuliwa siku aliyopeleka taarifa za mazungumzo aliyofanya na Mbowe.

Akijibu swali la Kibatala, shahidi alidai wakili atakuwa amekosea akisema walitunga kesi mapema kisha wakaanza kutafuta watuhumiwa.

Anadai hawakuwahi kujadili kumpeleka mtu kwa Mbowe akiwa na vifaa ili aweze kupeleleza na kurekodi.

Wakili Kibatala alitaka shahidi asema kama ni kweli aliambiwa na Mbowe atachukua nchi kwa namna yoyote na kama uchaguzi ulitajwa, akijibu; alidai anafahamu uchaguzi ulitajwa.

Shahidi anadai katika ushahidi wake hajasema mahali popote kwamba Mbowe alimtishia na alipoulizwa kwamba Mbowe alimwahidi cheo, alijibu kwamba hawezi kumpa cheo jeshini.

Anadai katika ushahidi wake hajawahi kumtaja Sabaya kutaka kudhuriwa, alitaja viongozi.

Luteni Urio anadai wakati anatafuta vijana alimpigia simu baba yake mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya kumwomba mwanawe akafanye kazi ya ulinzi kwa Mbowe.

Alidai baada ya Ling'wenya kukamatwa, baba yake alipiga simu kutaka kujua tatizo lililompata mwanawe alimjibu kwamba amuulize bosi wake.

Alikiri kwamba wakati anamwomba baba wa Ling'wenya hakumwambia kama kuna kazi kwa Mbowe lakini anataka akafanye mipango ya ugaidi.

Anadai mshtakiwa Halfani Bwire ambaye alikuwa akimpa taarifa hakumwambia maeneo gani mahususi ambayo walitembelea kwa ajili ya kumdhuru Sabaya.

Luteni Urio anadai hajui kama Adamu Kasekwa maarufu Adamoo na Ling'wenya walikamatwa maeneo ya Rau Madukani .

Wakili Kibatala alimwambia shahidi kuwa ni mtu muhimu kama yeye kupigiwa simu bila ridhaa yake anaweza kutoa taarifa lakini shahidi alijibu kwamba yeye si mtu muhimu.

Shahidi anadai maelezo aliyotoa Agosti 11, mwaka 2020 na anachosema kizimbani vinatofautiana.

Katika maelezo ya onyo ya mshtakiwa Ling'wenya ambayo anadaiwa alikiri, anadai Urio alimpa Sh. 87,000 na alimshauri mshahara uwe 800,000.

Shahidi alidai maelezo hayo si ya kweli na maelezo kwamba walipewa fedha zingine kwa ajili ya mavazi si kweli.

Shahidi huyo anadai wanatofautiana katika maelezo kwani yeye anasema aliwapa Ling'wenya na Kasekwa fedha kwa ajili ya kwenda Dar es Salaam, lakini Ling'wenya anadai aliwapa fedha kwa ajili ya kwenda Moshi.

Anadai hakuwahi kuambiwa na Inspekta Swila kuwa anastahili kuwa mshtakiwa wa kwanza au wa pili na kwamba DCI na ACP Ramadhan Kingai hawajamwambia kuwa watampatia kinga ya mashtaka.

Alipohojiwa kama Mbowe alimuomba amtafutie magaidi alijibu kwamba alimwomba amtafutie watu wa kwenda kufanya ulinzi.

Anadai Mbowe alitaja watu wa kufanya ulinzi ndio akawatafuta na hakumwambia akionana nao awaambie vipi lakini yeye alipowapata aliwaambia wanakwenda kufanya kazi ya ulinzi.

# Wanane upinzani kuchuana na Dk. Tulia uspika

**Salome Kitomari na Augusta Njoji,** DODOMA

WAGOMBEA wanane kutoka vyama vya upinzani ambao sio wabunge, wamejitokeza kuwania kiti cha Uspika wa Bunge kupambana na mgombea aliyethibitishwa na Kamati ya Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Tulia Ackson.

Dk. Tulia alithibitishwa jana kugombea nafasi hiyo, huku milango ya kumpata Naibu Spika ikitarajiwa kufunguliwa baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa spika.

Kikao Maalum cha wajumbe 340 kilichoongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kauli moja kilimpitisha Dk. Tulia na kwa upande wa nafasi ya Naibu Spika chama itatangazwa utaratibu baadaye baada ya kukamilishwa kwa uchaguzi huo.

Katibu wa Bunge ambaye ni Msimamizi wa Uchaguzi, Nenelwa Mwihambi, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, alisema hadi jana saa 10 jioni majina ya wagombea tisa yalishawasilishwa na kukidhi matakwa ya kisheria.

Alisema kati ya wagombea hao wanane si wabunge na mmoja ni mbunge ambaye ni Dk. Tulia. Aliwataja wagombea waliojitokeza na vyama vyao kwenye mabano ni Abdallah Mohamed Said (NRA), Aivan Maganza (TLP), David Mwaijojele (CCK), Georges Bussungu (ADA-Tadea), Kunje Mwiru (SAU), Maimuna Saidi Kassim (ADC), Ndonge Saidi Donge (AAFP), Saidoun Abrahmani Khatibu (DP), Dk. Tulia Ackson (CCM).

Uchaguzi wa Spika utafanyika leo baada ya wagombea hao kujieleza mbele ya wabunge na kupiga kura ya siri ya nani wa kukalia kiti hicho.

Baada ya kupatikana kwa Spika nafasi ya Naibu Spika inayoshikiliwa na Dk. Tulia itatangazwa kuwa wazi kugombewa.

Kwa upande wake, Dk. Tulia, akizungumza baada ya kuthibitishwa, aliishukuru Kamati Kuu cha CCM na Kamati ya Wabunge kwa imani waliyoonyesha kwake na umoja.

"Kwasababu mchakato huu wagombea tulikuwa 71 tunafahamu demokrasia ndani ya CCM mtu huruhusiwa baada ya chama kufungua milango ya kuchukua fomu, lakini anapochukua fomu anakuwa na watu wa hapa na pale wa kumpa ushauri kwenye mambo mawili, matatu."

"Niwatoe wasiwasi waheshimiwa wabunge yeyote ambaye anahisi alitoa ushauri eneo fulani au alionekana sehemu fulani na alionekana kuwa na mgombea kwenye mchakato, tunajua chama kina utaratibu na taratibu zote zinaheshimiwa, hivyo niwaombe sana kile cha kuwa na kauli moja tuendelee kuwa na kauli moja kwa yale yaliyo mbele yetu."

"Tumeamua kwa kauli moja kwenda pamoja, mchakato ni jambo la kawaida ndani ya chama kikubwa, hakuna sababu ya mbunge yeyote kujiona mnyonge kwa kuwa alikuwa akionekana na mgombea fulani, mimi nitakuwa kiongozi wenu nyie wote, asiwapo atakayejiona mnyonge kwa sababu yoyote ile kwa kuwa haya ni mambo ya mchakato," alisema.

Awali, Katibu wa wabunge hao, Rashid Shangazi, alisema zoezi hilo ni rahisi, lakini pia lina ugumu kwa kuwa wanamthibitisha mtu ambaye wanamfahamu na wamefanya naye kazi kwa zaidi ya miaka mitano.

"Ni gumu kwa kuwa lazima tufuate utaratibu kwa niaba ya chama chetu," alisema.

# Shirika lahamasisha chanjo UVIKO-19 kwa wanachama

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Liwale Socio-economic Development Organization, (LSED) la mjini Liwale mkoani Lindi, linalohamasisha kilimo cha alizeti, limegeukia uhamasiahaji wa chanjo ya UVIKO-19 kwa wanachama wake.

Mhamasishaji wa shirika hilo lisilo la kiserikali, Hassan Mpako, aliliambia gazeti hili jana kuwa ni mwezi mmoja sasa tangu waanze kazi ya kuhamasisha wanachama wao kujitokeza kuchanja.

"LSED imesajiliwa na serikali, hivyo ni haina budi kubeba ajenda za serikali ikiwamo ya kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya kujikinga na corona, ikiwa na kaulimbiu ya 'Chanjo ndiyo Mpango Mzima'," alisema Mpako.

Mpako alifafanua kuwa, kwenye uhamasishaji wa kilimo cha alizeti, wana kaulimbiu ya 'Alizeti na Pesa', na kwamba sasa wamekuja na hiyo nyingine ili kuhamasisha chanjo ya kujikinga na UVIKO-19.

Alisema, shirika hilo kwa sasa limeamua kufanya kazi hizo mbili kwa mpigo kama njia ya kusaidiana na serikali na wadau wengine katika vita dhidi ya ugonjwa huo unaoendelea kuangamiza watu duniani.

"Kama unafuatilia hali ya ugonjwa huo, utagundua kuwa kumekuwapo na mkanganyiko kuhusu suala la chanjo, tangu ulipoingia nchini, kwani wapo wasioona umuhimu wa kuchanjwa," alisema.

Alifafanua kuwa kutokana na sintofahamu hiyo, shirika hilo limeona kuna haja ya kusaidiana na serikali ya wilaya hiyo kuhamasisha wakulima na wananchi kwa ujumla, kuzingatia maelekezo yote kuhusu ugonjwa huo.

Mhamasishaji huyo alisema, shirika lake linajua kuwa suala la chanjo ni la hiari, na kwamba pamoja na hilo, kuna umuhimu wa kuelimisha jamii kutambua athari za ugonjwa huo, ili iamue kuchukua hatua sahihi.

Alisema, shirika lao lina wanachama 460 walioko katika kata 14 za wilaya hiyo, ambao wanahamasishwa kuchanja na kisha wenzao wanachukua elimu hiyo na kuisambaza wengine kwenye maeneo yao.

"Kama ambavyo tunaendelea na mpango wetu wa kuhamasisha kilimo cha alizeti kwa wakulima wote wilayani Liwale, ndivyo ambavyo pia tunataka tufanye kwenye suala uhamasishaji wa chanjo ya corona," alisema.

Akielekezea hatua ya shirika hilo, alipozungumza na gazeti hili, Mkuu wa wilaya hiyo, Judith Nguli, alipongeza kazi zinazofanywa na LSED na kusema zinalenga kuleta maendeleo ya wilaya hiyo.

"Kuhamasisha kilimo cha alizeti kunawafanya wakulima kuongeza zao lingine la kibiashara, na pia kuhamasisha chanjo, kunasaidia kuwafanya wakulima wawe salama na kufanya kazi za maendeleo," alisema Nguli.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wadau wengine wilayani humo kuiga mfano wa shirika hilo kwa kusaidiana na serikali katika vita dhidi ya ugonjwa huo.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, akifurahia jambo na watumishi wa wizara yake waliompokea katika hafla ya kilele cha magonjwa yasiopewa kipaumbele (Neglected Tropical Diseases), iliyofanyika jana viwanja vya Nyerere Square mkoani Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ACT yataka Baraza Kivuli la Mawaziri

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI Kuu ya Chama cha ACT - Wazalendo katika kikao chake kilichohitimishwa mwishoni mwa wiki, imeidhinisha azimio la kumtaka Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe, kuunda na kusimamia kamati itakayokuwa na jukumu la kutoa mbadala wa kisera na kuiwajibisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Halmashauri hiyo imemtaka Zitto kama msimamizi mkuu wa masuala ya sera wa chama awe ndiyo mwenye mamlaka ya kuunda na kusimamia kamati hiyo itakayoundwa chini ya azimio hilo.

Kupitia taarifa ya chama kwa vyombo vya habari jana, iliyotiwa saini na Katibu Mkuu wa chama, Ado Shaibu, ilibainishwa kuwa kamati hiyo ya kuisimamia na kuiwajibisha serikali itaundwa na wasemaji wa kisekta watakaotoa mbadala wa sera kwenye masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kitaifa na kimataifa.

Shaibu alifafanua kuwa moja ya masuala muhimu ya kimkakati ya Chama cha ACT - Wazalendo ni kuisimamia na kuiwajibisha serikali na tangu uanzishwaji wa mfumo wa vyama vingi serikali imekuwa ikisimamiwa na vyombo vya uwakilishi vikiwamo Halmashauri na Bunge.

"Utafiti uliofanywa na chama kupitia ziara mbalimbali za mikoani umeonyesha kuwa vyombo hivyo vimeshindwa kusimamia na kuwajibisha serikali ipasavyo bila shaka kwa kukosa uhalali wa kisiasa kwa sababu wajumbe wake wengi hawakuchaguliwa na wananchi," alisema Shaibu.

Alifafanua kuwa uchaguzi wa mwaka 2020 umeshuhudia vyombo hivyo kwa kiasi kikubwa vikikosa uwakilishi wa vyama vya upinzani ikiwamo kukidhi masharti ya kikanuni kuunda kambi rasmi ya upinzani ndani ya Bunge.

Zitto alipoulizwa lini anatangaza baraza hilo kivuli, alisema: "Ndani ya wiki hii nitakutana na wahariri wa vyombo vya habari na kutangaza wasemaji wa kisekta wa kila wizara ili kuongeza nguvu ya shabaha yetu ya kuwatumikia Watanzania kama chama cha siasa kisicho madarakani. Ni wajibu wetu kuisimamia serikali."

Utekelezaji wa azimio hili la Chama cha ACT - Wazalendo unaafikiana na hitimisho la kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Taifa kilichofanyika Oktoba 31, mwaka jana ambapo pamoja na masuala mengine, iliafikiwa kuwa mkakati wa chama mwaka 2021 mpaka 2025 ukamilishwe na uanze mara moja.


UBALOZI WA SWITZERLAND, NORWAY NA BRITISH HIGH COMMISSION DAR ES SALAAM

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Switzerland, Norway na British High Commission. watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Magari na Genereta tarehe 5 February, 2022 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set,Zanzibar beds, China base, Hutch, Chest drawer, Dining table, Book case, Office desk, Chairs,File cabinet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Upright Freezer, Washer, Dryer, A/c split units, Photocopy m/c, TV set, Computer set, Colour Printers, Safe cabinets,Steel Shelves, Aluminum Doors, Solar water heater, Lawnmower Na vingine vingi.

**Magari na Genereta yataanza kuuzwa saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser GX Station Wagon | 1HZ Diesel Engine | 2011 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser VX Station Wagon | 4.2TD Diesel Engine | 2005 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Patrol Y61 Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2010 | Umelipwa |
| 1 | Jeep Cherokee GH-KJ37 Station Wagon | KM31 Petrol Engine | 2003 | Umelipwa |
| 1 | Genereta 63 KVA Silence | Perkins Engine Diesel | 2012 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 2 mpaka 4 February, 2022, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Genereta atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 10 February, 2022 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.
7. Kila mtu anayesiriki mnada ni lazima kuvaa Barakoa na kunawa na maji tiririka au Sanitaiza, Umbali wa mtu na mtu uzingatiwe.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**Cell Number- +255 0754 284 926**
**Dar es salaam**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta:universalauctioncentre**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE , SIMU NA: +255 754 284 926,**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mikoa inayosuasua chanjo ya UVIKO-19 iige inayofanya vizuri*

**MWANZA** ni miongoni mwa mikoa mitano ambayo inatajwa kufanya vizuri katika chanjo ya UVIKO-19, ambapo Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Ruta Thomas, anataja sababu za mafanikio hayo.

Kwa mujibu wa Dk. Thomas, ushirikishaji wa wadau wote wakiwamo wahudumu wa afya kuanzia ngazi ya jamii na viongozi wa serikali za mitaa, kwa ajili ya uhamasishaji wa chanjo hiyo ni miongoni mwa siri ya mafanikio.

Vilevile, katika jitihada hizo za kufanikisha chanjo, anasema kuna kamati ya amani ya mkoa, ambayo iko chini ya viongozi kutoka madhehebu mbalimbali, inayohimiza amani na upendo, lakini inasaidia kuhamasisha watu kuchanja.

Pamoja na hayo, anasema, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza amekuwa akipokea taarifa za kila siku kutoka kila halmashauri ili kujua ni wapi kuna changamoto inayoweza kukwamisha chanjo, ili hatua zichukuliwe haraka.

Mbali na Mwanza mikoa mingine inayotajwa kufanya vizuri katika chanjo, ni Kagera, Mara, Dodoma na Ruvuma, inaonyesha kuwa bado kuna haja ya kuongeza jitihada zaidi ili kufanikisha chanjo hiyo.

Nchi ina mikoa zaidi ya 20, lakini inayotajwa kufanya vizuri ni mitano tu, kwa hali kama hiyo, tunadhani iko haja kwa mikoa ambayo iko nyuma kwenda kujifunza mbinu zilizotumiwa na mikoa ambayo iko juu kwenye chanjo.

Tunashauri hivyo, kwa sababu katika maisha ya kawaida, mbinu za kufanikisha jambo huwa zinatofautiana, hivyo kwenye suala la chanjo inawezekana baadhi ya mikoa ikawa kimbinu zaidi.

Lakini tunadhani kuna haja ya kukumbusha Watanzania kuwa nchi yao si kisiwa kisichofikika, bali ina mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali, hivyo kuchukua tahadhari ni jambo muhimu.

Hata Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anakiri kuwa mwitikio wa kuchanja bado ni mdogo nchini, ingawa matarajio ni kufikia asilimia 60 hadi mwishoni mwa mwaka huu, lakini waliochanja hadi sasa wakiwa ni watu 1,922,019.

Idadi hiyo inatajwa na Waziri Ummy kuwa ni sawa na asilimia 3.3 ya wale waliochanjwa, tangu chanjo zilipoanza kutolewa katikati ya mwaka jana ambazo ni aina ya Moderna, Johnson &Johnson, Pfizer na Synopham. Njia ambayo tunadhani inaweza kusaidia kufanya vizuri kwenye chanjo ni viongozi wa mikoa ambayo bado iko nyuma kwenda kujifunza kwa wenzao ambao wanatajwa kuwa juu kuhusu mbinu na mikakati waliyoibuni na kuitumia kufikia mafanikio hayo.

Tunajua kuwa chanjo ni hiari, lakini jambo la muhimu la kutambua ni kwamba, Tanzania si kisiwa ambacho hakifikiki, hivyo tunaona kuna umuhimu wa kila Mtanzania kupata chanjo ili kuwa salama zaidi.

Hivyo, mikoa hiyo inayotajwa kufanya vizuri kwenye chanjo, ingekuwa ni fursa kwa ile ambayo iko nyuma kujifunza mbinu na kwenda kuzitumia, ili wananchi wahamasike na kujitokeza kuchanjwa.

Kwa kufanya hivyo, tunaamini kwamba Watanzania wengi zaidi wanaweza kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu chanjo na kujitokeza kuipata, ili hatimaye lengo lililokusudiwa na serikali kuchanja asilimia 60 liweze kutimia.

Ni miezi sita sasa tangu chanjo ilipozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, lakini idadi ya waliochanjwa bado ni ndogo, hivyo tunaona kuna haja ya kuwakumbusha viongozi kwa mikoa ambayo inaendelea kusuasua katika chanjo, wachukue hatua zitakazowezesha watu wengi kuchanjwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Wahitimu sekta ya utalii, nchi imesheheni fursa zenu*

Na Christina Mwakangale

**BAADA** ya elimu kumpa mhitimu ujuzi aliouhitaji iwe ngazi ya astashahada au shahada matarajio wanaokuwa nayo wengi ni kuajiriwa. Lakini, kasi ya upepo zama hizi unahitaji juhudi zaidi zielekezwe kwenye wasomi hao kujiajiri.

Hatua hiyo ni muhimu kwa sababu ushindani ulioko sokoni kuziwania fursa finyu za ajira ni mkubwa, hivyo ubunifu, kujituma, kuwejikeania na kufikiri zaidi kutatua changamoto ya kazi vinafikiriwa kuwa vitaleta ahueni.

Wakufunzi wa Chuo cha Utalii cha Taifa (NCT), pamoja na wadau wa sekta ya utalii, hoteli wanazungumzia hayo na kuibua mbinu mpya kwa wahitimu wa chuo hicho, kwenye mdahalo kuelekea mahafali ya 19 yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, mwezi uliopita.

Wakufunzi wa chuo hicho, wanachosema ni kwamba hakuna ajira itakayowafuata watu bali wafanye juhudi kuitafuta, na hata kama wakijiajiri itawapasa kuwa wabunifu na shughuli zao kuwa za kipekee ili kukabili ushindani mkubwa sokoni.

Kinachohitajika ni bidii tangu wakiwa masomoni ili kufahamika na kuheshimika kutokana na kujituma. Ukijituma unapata ufadhili wa masomo unaweza pia kutumiwa na mashirika ya ndani na ya kimataifa. Lakini ukipata ajira msomi ni lazima uwe na nidhamu ya kazi ya hali ya juu na kuipenda kazi yako, kwa kuwa wenye elimu wengi wapo mtaani bila ajira.

Wahitimu siyo wa NCT pekee na wengine pia waibue mbinu za kukabiliana na changamoto kazini ambayo ni moja ya mafanikio, ikiwamo vijana kuyafahamu mazingira yao ya kazi, viongozi au mabosi wao pamoja na wateja wao.

Lakini hizi si zama za kukata tamaa ni kupambana hadi kieleweke, leo wengi wa wahitimu hukata tamaa mapema kutokana na ama mazingira magumu ya kazi au hata ukali wa mabosi ofisini, hilo si la kuwababaisha , lazima kujitahidi.

Pia kongamano linashauri kujikita katika eneo moja au kutoa huduma nyinginezo kwani kunamfanya mhitimu kujenga uzoefu na kuwa rahisi kutambulika.

Kwenye kongamano hilo, serikali inawapa neno wahitimu na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, anasema, wanatakiwa kutumia ujuzi walioupata kwa kujiajiri, badala ya kwenda kuwa mzigo kwa jamii na taifa kwa sababu ya kushindwa kutoe elimu kwa kukifanyia kazi kile walichokipata chuoni.

Masanja anasema kutokana na uhaba wa ajira wahitimu hao wasisubiri kuajiriwa serikalini pekee au sekta rasmi ikiwamo binafsi bali wajitumie alisema, "chagua moja kuajiriwa, au kujiajiri, usiende kuwa mzigo kule uendako. Ubunifu ni muhimu. Kwa miaka 60 ya Uhuru, hatujawahi kuwa na vazi rasmi, muwe wabunifu wa vazi hili ili kuitangaza Tanzania kikamilifu."

Kama waziri anavyobainisha fursa zinazohusiana na sekta hiyo zipo kuanzia ngazi za chini, kwenye vijiji, wilaya, mikoa na kitaifa na kwamba changamoto iliyoko sasa ni uhaba wa wataalamu wa kuandaa matukio na hafla mbalimbali, kuibua ubunifu na vitu vinavyovuta wengi na yote hayo yakilenga kujiajiri.

Licha ya serikali kuahidi kuwa itaendelea kuimarisha huduma zinazotolewa na sekta hiyo, ikiwamo mafunzo ya chuo kama cha NCT, ingawa UVIKO-19 umesababisha kuyumba kwa shughuli za kitalii na uchumi, vijana bado wanaweza kuchomoza na kujiajiri.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCT, Dk. Shogo Mlozi, anasema idadi ya wahitimu inaongezeka kila siku na mwaka huu wakiwa 541 na kwamba mkakati ni kutoa mafunzo ngazi ya shahada ili kupata wasomi na wajuzi zaidi wa sekta hiyo.

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WAFANYABIASHARA WANAOTAKIWA KUTUMIA MASHINE ZA EFD

**Dar es Salaam, Januari 31, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwatangazia wafanyabiashara wote na umma kwa ujumla kuwa, walipakodi wote wenye **mauzo ghafi yanayofikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni kumi na moja (TZS. 11,000,000) na kuendelea kwa mwaka** wanapaswa kununua na kutumia mashine za kutolea risiti za kielekitroniki (EFD).

Kwa mujibu wa **Kifungu namba 36**, kifungu kidogo cha (2) cha **Sheria ya Usimamizi wa Kodi Namba 438 ya mwaka 2015** iliyofanyiwa marekebisho mwaka **2019** inampa mamlaka Kamishna Mkuu kutangaza kwenye gazeti lenye mzunguko mkubwa aina ya wafanyabiashara wanaotakiwa kutumia mashine za risiti za kielekitroniki (EFD).

Hivyo, tunatoa muda hadi kufikia tarehe **28 Februari, 2022** wafanyabiashara wote wanaopaswa kutumia mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) kwa mujibu wa sheria na chini ya tamko hili, wawe wametekeleza maelekezo haya ndani ya kipindi hicho. Hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote watakaokiuka utekelezaji wa agizo hili.

Aidha, TRA inapenda kuwakumbusha pia watumiaji wa EFD ambao bado hawajazifanyia maboresho mashine zao ili kuendana na itifaki mpya ya mawasiliano ijulikanayo kama **Protocol 2.1** ili kutoa risiti za kielekitroniki zenye **"QR Code"** wawe wamefanya hivyo ndani ya muda uliyotolewa hadi kufikia tarehe **28 Februari 2022.**

Kwa msaada na maelezo zaidi, TRA inawahimiza wafanyabiashara na umma kwa ujumla kutembelea katika Ofisi za TRA zilizo karibu, au tovuti ya TRA www.tra.go.tz au Kituo cha Huduma kwa Mlipakodi kinachopatikana kwa namba za kupiga bure "Toll free" 0800 750 075 au 0800 780 078 au barua pepe huduma@tra.go.tz

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**A.J. Kidata**
**KAMISHNA MKUU**

# ‘Marufuku kuwatoza wajawazito’

**Na Boniface Gideon,** TANGA

BAADA ya kuwapo kwa manung’uniko kuhusu wajawazito kutozwa kodi wakati wa kliniki kwenye hospitali za umma, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu amepiga marufuku.

Jana kwenye ziara yake ya kushtukiza katika Kituo cha Afya Makorola, Waziri Ummy alipokea malalamiko hayo na kuwauliza wataalamu wa afya, ambao walikiri kuwatoza wajawazito 31 kwa ajili ya vipimo vya afya.

Waziri Ummy aliomba kupata msaada wa kisera kutoka kwa wataalamu wa wizara ikiwa sera ya afya imebadilishwa kwa wajawazito.

“Nimepiga simu kwa wataalamu wa wizara, sera ya afya nchini bado haijafanyiwa mabadiliko yoyote kwa wajawazito huduma zao ni bure, nielekeze nchi nzima kuwa matibabu kwa wajawazito ni bure, tunataka tutokomeze vifo vitokanavyo na ujauzito visiwapo kabisa hapa nchini,” alisisitiza Ummy.

Aliwataka wahudumu wa afya nchini kwenye hospitali zote za umma kutoa huduma bure kwa wajawazito iwe kupima au kuhudhuria kliniki.

“Sidhani kama inaingia akilini eti mtu atoke huko aje hapa aseme ni mjamzito ukawa ni uongo, Sera ya Afya haijafanyiwa mabadiliko yoyote bado inatoa huduma ya afya kwa wajawazito bure, wasitozwe chochote,” alisisitiza Waziri Ummy.

Kadhalika aliiagiza Halmashauri ya Jiji la Tanga kupitia mkurugenzi kununua jenereta kwenye Kituo cha Afya Makorola ndani ya siku tano ili kukidhi mahitaji ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

“Hospitali inafanya huduma za dharura mpaka usiku na sasa hivi tumeambiwa kuna mgawo wa umeme unakuja, naelekeza nataka jenereta linunuliwe na liletwe kwenye kituo cha afya, nasema ndani ya siku tano nataka jenereta liwe limefika, nataka wananchi wanaotumia huduma katika kituo hiki wazipate bila kikwazo, jenereta lije ndani ya siku tano,” aliagiza.

Pia alisema ni vyema waganga wakuu wa wilaya wakapewa maelekezo nini serikali ya awamu ya sita inataka.

“Tuwaelekeze waganga wakuu wote wa wilaya matarajio ya serikali ya awamu ya sita kuwa ni huduma bora, tunaweza tukawa na majengo mazuri, lakini watu wakafa kutokana na huduma mbovu, majengo mazuri sio ubora wa huduma ya afya, tunataka majengo mazuri tuliyojenga yaendane na ubora wa huduma bora za afya,” alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel (katikati), akijadiliana jambo na Mbunge wa Jimbo la Magu, Boniventure Kiswaga (kulia), baada ya kufanya kikao kazi jana na watumishi wa idara ya misitu. **PICHA: ROSE JACOB**

# Askofu Ruwa’ichi akataza simu kwenye ibada

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Dar es Salaam, Mhashama Jude Thadaeus Ruwa’ichi, amewataka waumini wa kanisa Katoliki kuacha kuhangaika na simu wakati wa ibada.

Askofu Ruwa’ichi alitangaza katazo hilo juzi wakati wa uzinduzi wa Kanisa la Mtakatifu John Boosco lililoko Tumbi Kibaha, lenye uwezo wa kuhudumia waumini 1,400, huku akisema ni lazima waumini wabadilike na kuheshimu sehemu ya ibada.

Alisema lengo la kwenda kanisani lisiwe ni kupiga picha wala kuhangaika na simu badala yake kazi hiyo waachiwe wanaohusika na baadaye anayetaka ataomba atumiwe.

Askofu Mkuu huyo alisema ma kanisa ni nyumba ya Mungu mahali patakatifu kukaa watu watakatifu, hivyo ni vema pakaheshimiwa.

“Kila mahali pana heshima yake, nyumba ya Mungu iheshimiwe itumike vyema na watu wa Mungu kwa ajili ya ibada ya neno la Mungu, na tuendelee kumuabudu Mungu kwa haki na ukweli,” alisema.

Alisema kanisa zuri ni kwa ajili ya Wakristo wazuri, hivyo ni vyema waumini wakawa na matendo mazuri yanayoendana na kanisa hilo.

Aliwapongeza waumini kwa kujitoa kwa michango ambayo imefanikisha ujenzi wa kanisa hilo, na kwamba ni jambo la kuigwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Parokia hiyo, Michael Ntambi, alisema kanisa hilo lilianza kujengwa Aprili 2009 na hadi kukamilika limetumia zaidi ya Sh. bilioni 2.

Ntambi alisema fedha hizo za ujenzi ni kutoka kwa waumini na marafiki wa Parokia na kwamba kanisa la awali lilikuwa na uwezo wa kuingiza watu 200.

# Kampeni NMB MastaBata Kivyako Vyako yasisitiza kadi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kampeni ya NMB MastaBata - Kivyako Vyako ikizidi kunufaisha wateja kwa washindi 25 wa mwezi wa kwanza wa kampeni hiyo kuzawadiwa Sh. milioni 25, msisitizo umetolewa kwa Watanzania kuwa matumizi ya pesa taslimu ni gharama na kwamba MastaBata ikawe chachu ya kudumisha utamaduni wa matumizi kwa njia ya kadi.

MastaBata ni kampeni inayoendeshwa na Benki ya NMB, ikihamasisha Watanzania kuendana na kasi ya dunia ya dijitali ya matumizi ya yasiyohusisha pesa taslimu, huku benki hiyo ikitenga zaidi ya Sh. milioni 200 kama motisha kwa wateja wanaotumia zaidi kadi zao za MasterCard, Masterpass QR, Vituo vya Mauzo (PoS).

Kufikia sasa, kampeni hiyo iliyoanza mwishoni mwa Desemba mwaka jana, imeshatoa zawadi za pesa taslimu kiasi cha Sh. milioni 65 kwa wateja 425, ambazo ni kati ya zaidi ya Sh. milioni 200, zitakazotolewa kwa wateja 1,080 katika kipindi cha wiki 10 za kampeni hiyo, inayofanyika kwa msimu wa tatu. Fainali ya NMB MastaBata itafanyika Machi mwaka huu.

Akizungumza kabla ya droo hiyo, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema ulimwengu umebadilika na kusisitiza kuwa matumizi ya pesa taslimu yana gharama kubwa, zikiwamo za upotevu, wizi na uporaji na kwamba Watanzania wanapaswa kuendana na kasi ya mabadiliko hayo kwa kujikita katika matumizi kwa njia ya kadi.

“Upo msemo usemao ‘cash is expensive’ yaani matumizi ya pesa taslimu ni gharama sana kwa sababu kutembea na pesa kwenda ‘supermarket, vituo vya mafuta, madukani, migahawani na kwingineko ni hatari, unaweza kupoteza pesa, kuibiwa ama kuporwa.

“Katika kuendana na mabadiliko hayo, kwa msimu wa tatu sasa NMB tukajikita katika kuhamasisha matumizi na manunuzi kwa njia ya kadi, ambako tukaona tusiende na kampeni hii mikono mitupu, ndipo tukaja na motisha za viwango mbalimbali kwa wateja wetu kote nchini.

“Licha ya faida ya usalama na unafuu watakaopata kwa kutumia kadi zao kufanya malipo na manunuzi, pia wateja wetu watanufaika na zawadi za pesa taslimu tunazotoa kwa wiki, mwezi na katika fainali. Ni kampeni chanya ambayo imetupa NMB tuzo ya kuwa benki kinara wa kuhamasisha matumizi hayo tuliyopewa na MasterCard International,” alisema Donatus.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa NMB, Aikansia Muro, alisema benki yake imetenga zaidi ya Sh. miliono 200, zitakazotolewa kwa wateja wao katika kipindi chote cha kampeni hiyo, ambako kila wiki wateja 100 hujinyakulia jumla ya Sh. milioni 10 (sawa na Sh. 100,000 kila mmoja), huku washindi 25 wa kila mwezi wakijitwalia Sh. milioni 25 (sawa na Sh. milioni 1 kila mmoja).

**HABARI KITAIFA**

# 1,544 wahamishwa vituo vya kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WATUMISHI 1,544 wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa wamepewa uhamisho vituo vya kazi baada ya maombi yao kuridhiwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe. Prof. Shemdoe amesema TAMISEMI inaendelea kufanyia kazi uhamisho wa kubadilishana kwa sasa.

"Wale walioomba uhamisho usio wa kubadilishana vituo kuanzia Julai, 2021 hadi Januari, 2022 kwenda halmashauri za wilaya waendelee kusubiri wakati tathmini kwenye halmashauri zote ikiendelea kufanyika ili kufanya msawazo," alisema Shemdoe.

Pia aliwataka watumishi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa waliowasilisha maombi yao ya uhamisho OR-TAMISEMI kwa kipindi cha Januari 2018 - Juni 2021, kuomba upya kuhamia kwenye maeneo hayo lakini isiwe kwenye majiji, manispaa na halmashauri za miji.

Alisisitiza maombi hayo yazingatie utaratibu wote wa uhamisho kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Uhamisho Na. 2 wa mwaka 2018.

Halikadhalika, aliwataka watumishi waliopata vibali vya uhamisho kusubiri barua kwenye halmashauri zao badala ya kwenda Ofisi ya Rais-TAMISEMI kufuata barua hizo na kuwa orodha ya majina ya watumishi waliopata vibali vya uhamisho inapatikana kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI www.tamisemi.go.tz

Alisema endapo mtumishi atakuwa na changamoto yoyote asisite kupiga simu kwenye Kituo cha huduma kwa mteja kwa namba za simu: +255735-160210, +255262-160210 ama kuandika barua pepe kwenye anwani yetu ya huduma@tamisemi.go.tz.




Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Mtinika akipokea sehemu ya vifaa vya kufanyia usafi kwa Meneja Uhusiano wa Benki ya Biashara ya DCB, Brino Londo (wanne kushoto), katika siku ya usafi ya mwisho wa mwezi iliyofanyika kiwilaya katika kata ya Keko jijini Dar es Salaam jana. DCB imeshiriki kampeni hiyo kupitia mfuko wake wa kusaidia jamii wa DCB Foundation kwa kufanya usafi na kukabidhi msaada wa vifaa vya kufanyia usafi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mfumo dirisha la pamoja kwa wawekezaji wanukia

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WATAALAMU wanaojenga mfumo wa dirisha la pamoja la kuhudumia wawekezaji la kielektroniki Tanzania (TeIW) wamepongezwa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika awamu ya kwanza ya ujenzi.

Wataalamu hao wamepongezwa na viongozi wa taasisi za serikali zinazotoa vibali, leseni na huduma mbalimbali kwa wawekezaji chini ya Kituo cha Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Centre [OSFC]) baada ya mkutano wao katika Ofisi ya Waziri Mkuu jijini Dodoma.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo wa viongozi, Mkurugenzi Mtendaji wa TIk, Dk. Maduhu Kazi, alisema viongozi wanaamini awamu ya kwanza ya ujenzi wa dirisha hilo utakwisha Februari 28 kama inavyotarajiwa.

"Tumeridhishwa na kufurahishwa na kazi ambayo tayari imefanyika. Tumewahimiza wataalamu wetu waendelee kwa kasi na ari ile ile ili tufikie lengo la kumaliza awamu ya kwanza Februari 28," alieleza Dk. Kazi. Ujenzi wa mfumo huo mpaka jana ulikuwa umefikia asilimia 42 ya utekelezaji.

Alifafanua kuwa TeIW ni suluhisho la mtandao ambalo linalenga kuwezesha na kurahisisha upokeaji wa maombi, utoaji wa huduma za vibali, leseni na usajili kwa wawekezaji kwa haraka.

"Lengo la mfumo huo ni kurahisisha mtiririko wa taarifa kati ya taasisi zote zilizoko ndani ya OSFC." Dk. Kazi alieleza kuwa mfumo huo, ambao unafadhiliwa pia na Taasisi ya TMEA, utakuwa ni hazina ya taarifa zote muhimu kwa ajili ya uwekezaji kwa wadau wote wanaohitaji kuwekeza Tanzania na kuongeza kuwa utatekelezwa kwa awamu tatu ambapo kwa kuanzia utahusisha taasisi za TRA, BRELA, Kazi, Uhamiaji, NIDA, Ardhi na TIC.

Jumatano, Kamati ya Kuhudumia Uwekezaji ya Taifa (NIFC), ambayo uhusisha taasisi za serikali zinazotoa vibali, leseni na huduma mbalimbali kwa wawekezaji, ilijadili maendeleo ya TeIW ilipokutana na kuamua kuwatembelea wataalamu wanaojenga mfumo huo.

# Wananchi watenga hekari 58 kujenga sekondari

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

UKOSEFU wa shule ya sekondari katika kata ya Puni, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, umesababisha baadhi ya wanafunzi hasa wa kike kuacha masomo na kubaki nyumbani baada ya kutembea umbali wa kilometa 10 kwenda na kurudi Shule ya Sekondari ya Itwangi, Kata ya Nyida.

Kutokana na ukosefu huo, wananchi wamelazimika kutenga zaidi ya hekari 58 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya kata kusaidia kuondoa tatizo hilo.

Wakazi wa kata hiyo waliwambia mwandishi wa habari hizi kwa nyakati tofauti, wakati wa utekelezaji wa mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na Klabu cha Waandishi wa Habari mkoa wa Shinyanga (SPC) kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mmoja wa wakazi hao, Happynes Kishimba alisema, kata hiyo haina sekondari, wanafunzi wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 10 kwenda na kurudi kutafuta elimu katika Sekondari ya Itwangi iliyopo kata ya jirani ya Nyindo na kusababisha wanafunzi kushindwa kuhitimu masomo yao.

Alisema, wanafunzi wa kiume wanaongoza kwa kuhitimu elimu za msingi na sekondari ikilinganishwa na wanafunzi wa kike na kuomba serikali kutafutia ufumbuzi suala hilo.

Mkazi wa kata hiyo, Amos Daudi alisema, sababu nyingine ya wanafunzi kuacha masomo ni adhabu zinazotolewa na walimu shuleni kwa kucharazwa bakora zaidi ya 10 mikononi na kuingiwa na woga na kuacha masomo yao moja kwa moja na kubaki nyumbani.

"Mimi mwenyewe mjukuu wangu alikuwa anasoma kidato cha tatu Sekondari ya Itwangi, alipigwa bakora akaja amevimba mikono na kwa muda wa wiki nzima tulikuwa tunamlisha chakula kama mtoto mdogo, baada ya kupona aliacha shule na kukimbilia kwa shangazi yake Sengerema," alisema Daudi. Kwa upande wake, Ofisa Elimu Sekondari wa halmashauri hiyo, Stewart Makali, alisema kati ya kata 26 kwenye kata za Puni na Usule hazina shule za sekondari na juhudi za kuhakikisha zinakuwa na sekondari zinafanyika.

Alisema, mpango wa kitaifa wa serikali ni kujenga shule 1,000 za sekondari nchi nzima, kati ya hizo wamepata mbili zitakazojengwa kata hizo na Kata ya Usule ujenzi unaendelea baada ya wananchi kuonyesha juhudi za kuchangia vifaa vya ujenzi.

Makali alisema, sera ya elimu inataka kila kijiji angalau kuwe na shule ya msingi na kata kuwe na shule ya sekondari kulingana na mahitaji.

# Waziri: Kabilianeni na vikwazo vya mazingira

**Na Rose Jacob,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amewaomba viongozi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kuchukua hatua za haraka kukabiliana na vikwazo mbalimbali katika masuala ya uhifadhi wa mazingira.

Alitoa rai hiyo jana baada ya kupokea taarifa ya hali ya uhifadhi mkoani Mwanza na kuitaka jamii za wakulima na wafugaji zinazoishi maeneo ya hifadhi za misitu kuishi kwa amani na kuhifadhi mazingira kwa faida ya vizazi vijavyo.

Masanja alisema miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili wananchi wa vijiji vinavyouzunguka misitu nchini ni pamoja na elimu juu ya uhifadhi na athari zake, namna wanavyoweza kutumia hifadhi za misitu kutokomeza umaskini pamoja na kutokuwapo matumizi bora ya ardhi.

"Natoa rai kwa uongozi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFSO, viongozi wa wilaya na vijiji kushirikiana pamoja kuelimisha wananchi wanaozunguka hifadhi za misitu, wakala watafute namna ya kuanzisha miradi kupitia programu za kurudisha kwa jamii ili kusaidia jamii iliyopo kando mwa misitu," alisema Masanja.

"Ninafahamu kuwa kuna kamati ya mawaziri nane iliyoundwa kushughulikia migogoro ya mipaka katika hifadhi za misitu, lakini wakati tukishubiri kamati hiyo kutoa mapendekezo yake, tuanze sasa kutoa elimu na kuwafanyia vitu vingi vya CSR ikiwamo kuwapelekea miradi ya ufugaji nyuki, kilimo na ufugaji bora ili watuelewe na wajue tunapohimiza uhifadhi tuna lengo zuri," alisema Masanja.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema misitu iliyoko mikoa ya Kanda ya Ziwa haina hali nzuri na kuwataka viongozi kuchukua hatua za kuhimiza uhifadhi.

"Msitu yetu tumeiona kwenye ramani kubwa hapa niwaombe viongozi tuwe na moyo wa kihifadhi, kanda hii kuna maeneo yalikuwa na mvua mara mbili kwa mwaka na sasa mvua ni za kubahatisha, maeneo mengine yanakumbwa na ukame, hakuna muujiza ni uhifadhi, kuna maeneo yalikuwa na mito mikubwa sasa imekauka ng'ombe wamekufa, tuna haja kubwa ya kuwekeza kwenye mabadiliko ya tabia nchi," alisema Gabriel.

Aliwataka viongozi wakiwamo wabunge na wale wa serikali kuu kuimba wimbo mmoja, ili kushirikiana kuhifadhi misitu kwa faida ya kizazi kijacho.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, alisema kuna haja ya kuwepo programu ya kutoa mafunzo ya uhifadhi sambamba na kuanzisha miradi yenye manufaa katika uhifadhi wa misitu.

Kwa upande wake, Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema wapo tayari kushirikiana na viongozi wa mikoa ya kanda ya ziwa kuhakikisha uhifadhi unafanikiwa.

Aidha, alisema licha ya matatizo mbalimbali yaliyoko katika sekta ya uhifadhi nchini, TFS itahakikisha kunakuwapo na usimamizi endelevu wa raslimali za misitu na nyuki ili kuchangia mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiikolojia na kiutamaduni kwa kizazi cha sasa na kijacho.



Mwanakijiji Kuzenza Maguta na wenzake wakiangalia uharibifu uliofanywa na tembo baada ya kuvamia shamba la Dionitz Buhuta na kuharibu mahindi katika kijiji cha Ngaralambe wilayani Biharamulo mkoani Kagera hivi karibuni. **PICHA: RENATUS MASGULIKO**

# TAKUKURU yaonya uhujumu wa miradi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, amewaonya watu wenye nia ya kuihujumu Serikali kwenye miradi ya maendeleo kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Suzana alitoa kauli hiyo mjini Kibaha alipokuwa akitoa taarifa ya miezi mitatu ya Taasisi hiyo kwa waandishi wa habari.

"Tutakuwa wakali sana kwa watu wanaojihusisha na rushwa au ufisadi kwenye miradi ya maendeleo, tuungane pamoja kujenga Tanzania yenye maendeleo ya kweli kupitia miradi hiyo inayoanzishwa na Serikali yetu," alisema Suzana.

Aliwaomba wakazi wa Mkoa wa Pwani kufuatilia miradi ya maendeleo katika maeneo yao na kutoa taarifa p wanapokuwa na shaka kuhusiana na utekelezaji wa miradi hiyo.

"Katika usimamizi wa miradi tutangulize uzalendo tuwe waaminifu na waadilifu ili kujenga Tanzania imara kadri ya maelekezo ya serikal," alisisitiza.

Alieleza kuwa katika kipindi cha miezi mitatu miradi ya maendeleo 56 katika sekta za afya, elimu na maji yenye thamani ya Sh. bilion 11.9 ilikaguliwa.

Alisema katika ukaguzi mapungufu yaliyobainika yalifanyiwa marekebisho ili kuhakikisha miradi inalingana na thamani ya fedha.

Katika kipindi hicho pia malalamiko 132 yalipokelewa katika taasisi hiyo ambapo kati ya hayo 93 yalihusu rushwa, na kwamba 92 uchunguzi wake unaendelea na moja uchunguzi umekamilika.

## Kunenge: Viwanda visaidie jamii jirani

**Na Julieth Mkireri,** PWANI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka wawekezaji wa viwanda katika mkoa huo kuhakikisha wanasaidia jamii inayowazunguka.

Kunenge, ametoa kauli hiyo juzi alipokuwa katika kiwanda cha Prance International Trade Co LTD kilichoko eneo la Saeni Kata ya Misugusugu Kibaha Mjini alipokuwa katika ziara yake ya kutembelea viwanda.

Akiwa katika kiwanda hicho kinachozalisha vifaa vya ujenzi ikiwamo misumari, waya aina zote, sabuni ya Nice One na taulo za watoto, alisema pamoja na serikali kunufaika na uwekezaji katika kukuza uchumi, pia jamii inayozunguka inatakiwa kunufaika.

Kunenge, alikipongeza kiwanda hicho kwa kujitoa katika kusaidia jamii na kwamba tayari wameonyesha mfano wa kuchangia saruji mifuko 400 kwa ajili ya kuchangia ujenzi Zahanati ya Mtaa wa Saeni.

Aliwataka wawekezaji hao kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia sera na sheria za nchi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima baina ya serikali, taasisi, wananchi kwa kuwa nchi bado inawahitaji kwa kiasi kikubwa wawekezaji.

Ofisa mwajiri wa kiwanda hicho, Noel Mwasajone, aliishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji huku akiomba changamoto ya umeme na barabara zifanyiwe kazi.

## Wanufaika TASAF wafurahia maji

**Na Elizabeth Zaya**

WALENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wameelezea namna mradi wa kuchimba mabwawa ya maji ulivyowasaidia kupunguza tatizo la maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwamsundi, Mkata wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga, Hosen Mkangara, alisema mpango huo wa kuchimba mabwawa ni miongoni mwa miradi ambayo inatekelezwa na TASAF na inafanywa na walengwa wa mpango huo kama ajira za muda za kuwaongezea kipato.

"Tunashukuru sana, mbali na kwamba mradi huu wa kuchimba mabwawa uliletwa na TASAF kwa ajili ya kuwanufaisha walengwa wao kupitia ajira za muda, lakini umefanyika mkombozi kwa wananchi wote wanaouzunguka, kabla ya kuletwa mradi huu tulikuwa tunahangaika sana na maji, lakini kwa sasa tatizo hili limepungua sana," alisema Mkangara.

Alisema zaidi ya vijiji vitano vinavyozunguka mabwawa hayo yaliyochimbwa na walengwa alimaarufu kama marambo, wananufaika na maji hayo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 1, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Joto la nishati makaa ya mawe kuleta mwisho wa dunia**



Ukurasa 12

Ni kichefuchefu mabanda ya taka yakielemewa na uchafu



Ukurasa 13

LHRC, Wajapani wanapojitosa kuukabili unyanyasaji kingono sekondari na msingi

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Walengwa TASAF vijijini wanapoibua vilio, vikwazo malipo kwa njia ya simu

• Hawajui kusoma, kuandika, kutoa pesa



Justina Malale, Mlengwa wa mfuko wa TASAF kutoka Kijiji cha Nzonza, Shinyanga,akielezea changamoto ya mfumo mpya wa malipo kwa simu. **PICHA: MARCHO MADUHU**

KUTOKUJUA kusoma na kuandika lakini uelewa mdogo wa matumizi ya teknolojia za habari na mawasiliano, kumewaibua baadhi ya wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini mkoani Shinyanga, wakisema itakuwa changamoto kupokea fedha zinazotumwa kwao kwa simu kwa sababu hawataweza kuzitumia.

Mpango huo unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ili kuzisaidia familia zisizo na uwezo wa kujikimu kwa kuzipatia fedha, hivi karibuni umetangaza kuwa utaanza kutoa malipo kwa simu kwa walengwa wa vijijini na kupitia benki kwa wanaoishi mijini.

Wanufaika wanasema baadhi, hawajui kusoma wala kuandika tena sio wote wenye simu za mikononi. Wahitaji hao hupewa fedha kila baada ya miezi miwili, ili kupeleka watoto shuleni, wadogo kliniki, kupata bima ya matibabu (CHF) na kuanzisha miradi ya uzalishaji mali ili wajipatie kipato na kuondoa umaskini, kupitia TASAF 111.

Wanaoishi vijijini, pamoja na madai ya kutomiliki simu, kushindwa kusoma na kuandika wana jingine kuwa maeneo hayo hakuna huduma ya mawakala wengi wa kuwafikishia wananchi wengi huduma za fedha kwa njia za mtandao wa simu.

Baadhi ya wanufaika wanaoishi katika vijiji vya Buduhe na Nzonza wilayani Shinyanga, ni miongoni mwa wanaokiwakilisha kilio hicho cha mfumo mpya wa malipo kwa simu katika maeneo mengi ya vijijini hapa nchini.

Pelanya Mashamba anayeishi Nzonza, analalamikia mfumo huo mpya wa malipo kwa njia ya simu, kuwa wazee wengi maeneo ya vijijini hawamiliki simu na wala hawajui kusoma na kuandika, hivyo kulipwa fedha zao kwa njia ya simu ni tatizo jingine.

Suzana Shija kutoka Buduhe anamuunga mkono akisema maeneo mengi ya vijijini hakuna mawakala wa M-Pesa, Tigo-Pesa, Halo Pesa au Aitel Money na kwamba wakati mwingine wanalazimika kutembea kilomita tano kwenda eneo lenye mikusanyiko ya watu wengi au senta ili kupata huduma hiyo.

“Mfumo huu mpya wa malipo ya fedha za TASAF kupitia simu, kwa walengwa vijijini ni shida kwa sababu wengine hatumiliki simu na hata kama tukisema tununue wapo wasiojua kusoma, kuandika tena ni wazee bila kusahau umbali wa kufika eneo la kutolea pesa,” anasema Suzana.

“Tanaiomba serikali itutazame tena sisi tuliopo maeneo ya vijijini tuendelee kupewa fedha zetu kama zamani, kwa kuzifuata kwenye ofisi za kata, lakini malipo kwa simu itakuwa vigumu hatutaweza,” anaongeza.

Helena Makoye mkazi wa Kijiji cha Buduhe wilayani Shinyanga, anasema mfumo huo utawaathiri wasiojua kusoma na kuandika kama yeye, “mimi siyo kwamba sina hela ya kununua simu ni nazo, ninao kondoo nane, lakini tatizo sijui kusoma na kuandika ukimpatia mjukuu akakutolee anaweza kutumia baadhi na akakundanganya, tunaomba tuendelee kupokea malipo kwa mfumo wa zamani tu,” anasema Helena.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Buduhe, Masanja Samike, anaunga mkono mfumo wa kulipa fedha kupitia ofisi za kata kutokana na changamoto wanazozitaja kwa kuwa wengi ni wazee.

Anasema fedha za TASAF zimekuwa msaada mkubwa sana kwa walengwa ambao wanaishi kijijini humo, ambapo maisha yao yamebadilika tangu walipoingia kwenye mpango huo, na baadhi yao wanamiliki mifugo, mashamba, nyumba, na wanasomesha watoto hadi vyuo vikuu na wanahitaji kuendelea kuungwa mkono na serikali.

“Suala la mfumo mpya wa malipo ya walengwa wa TASAF kwa njia ya simu litizamwe hasa kwa maeneo hayo ya vijijini, sababu idadi kubwa ya wanufaika hawana simu na hawajui kusoma, kuandika na hakuna vibanda vya huduma ya kutoa pesa jirani na makazi yao”. Anasema Samike.

### MSIMAMO WA TASAF

Mratibu wa TASAF mkoani Shinyanga, Dotto Maligisa, anatolea ufafanuzi mfumo huo mpya wa malipo ya walengwa wa TASAF kwa njia ya simu na benki, kuwa ni kupunguza gharama za uendeshaji kwa kulipa posho waleta fedha vituoni na mafuta kwenye magari.

Anataja sababu nyingine, kuwa ni kuwapunguzia walengwa changamoto ya kutoka umbali mrefu kuja kituoni kuchukua fedha, huku wengine wakiwa na matatizo ya miguu, wapo na wenye ulemavu, lakini kwa mfumo huo mpya watakuwa wakipokea fedha zao wakiwa nyumbani kwa njia ya simu.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MWANDISHI WETU, SHINYANGA

# Ni kichefuchefu mabanda ya taka yakielemewa na uchafu

KUKOSEKANA teknolojia na utaalamu wa kuzoa taka kwa gharama nafuu ambayo pia ingeweza kuwa ajira kwa vijana, kumeendelea kuwatesa wakazi wa mitaa iliyo karibu na nyumba za kuhifadhia taka au maghuba katika maeneo mengi ya Manispaa ya Shinyanga.

Kwa miaka mingi hakujawa na ubunifu wa kutumia mbinu nyingine za kuzoa taka mbali na kutegemea magari, vijiko na mikokoteni kuikusanya na kuzirundika mitaani ambazo zinapoachwa bila kuzolewa, zinageuza maisha ya wananchi wanaishi jirani nazo kuwa adhabu kutokana na kuzalisha vimelea vya magonjwa, wadudu kama panya, kutiririsha maji yake na kuhatarisha usalama wa afya za familia kuanzia watoto, wazee pamoja na mazingira.

Sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004, inasema kila mtu anayeishi Tanzania ana haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya, lakini katika Manispaa ya Shinyanga hali ni tofauti, ambapo kuna usugu wa uzoaji taka kwenye nyumba za kukusanyia taka ili kuzipeleka dampo.

Nipashe imetembelea maeneo ya Shinyanga ambayo yana nyumba hizo za kuhifadhia taka na kukuta hali ni mbaya zikiwa zimejaa kupindukia na kusababisha kutapakaa hadi nje na kuzagaa kwenye makazi ya watu, na kusababisha malalamiko kuwa zinahatarisha afya za wananchi.

Moja ya eneo ambalo taka zimekaa muda mrefu tangu Novemba mwaka jana ni ghuba lililoko Mtaa wa Mapinduzi, Kata ya Ndala huko kuna harufu mbaya, inzi, funza, maji machafu na kuwa tishio kwa afya za wananchi hasa wale ambao wanaishi jirani.

Rehema Mussa ni mkazi wa Mapinduzi, ambaye anaishi jirani na uchafu, anasema afya zao ziko hatarini hasa katika kipindi hiki cha mvua, kutokana na maji machafu kutiririka kutoka kwenye ghuba hilo na kwenda kwenye makazi yao muda wote.



Ghuba la taka kwenye Mtaa wa Mapinduzi mjini Shinyanga. **PICHA: MWANDISHI WETU**

> Siyo kwamba manispaa tunapenda hali hiyo, bali ni changamoto za ubovu wa magari yetu ya kuzolewa taka, pamoja mtambo au kijiko na kuzipakia kwenye kijiko, ndiyo sababu kila mahali kumeelemewa na uchafu.

Anasema wakati wa kula kuna shida mbali na kujaza inzi kwenye vyakula, kuna harufu kali inayowakera na kuiomba serikali, iweke utaratibu wa kuzoa uchafu huo mara kwa mara na siyo kuacha marundo hayo kuchukua siku nyingi mitaani na kuhatarisha afya zao kwa kusababisha uwezekano wa magonjwa ya milipuko.

"Uchafu unapokuwa mwingi bila kuzolewa kwa wakati, ni hatari sana hasa sisi wananchi ambao tunaishi jirani na maghuba haya pamoja na watoto wetu sababu wamekuwa wakichezea uchafu huo, kilio chetu kwa serikali ituzolee uchafu huu ili tubaki kuwa salama hasa kipindi hiki cha mvua ambacho kuna uwezekano wa milipuko ya magonjwa,"anasema Mussa.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mapinduzi, Zabibu Cosmas, anasema ghuba hilo linazaidi ya miezi mitatu, taka hazijazolewa na kupelekwa dampo, na viongozi wameshatoa taarifa mara kwa mara kwa uongozi wa Manispaa ya Shinyanga, lakini hakuna utekelezaji na wananchi wakiendelea kuwa hatarini.

Anasema viongozi wa mtaa hawana uwezo wa kuzizoa taka hizo, na kwamba ni jukumu la halmashauri, ikiwa wao ndiyo wenye bajeti na kandarasi za wenye magari ya kuzolea taka na kupeleka dampo.

"Ifahamike kuwa wananchi wa eneo hili la Mapinduzi wakipatwa na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu si wao tu watakaoathirika, bali kitaenea kwa watu wengi hata mbali ya Shinyanga na kuleta madhara makubwa, Waswahili wanasema kinga ni bora kuliko tiba, hivyo naomba uchafu huu uzolewe,"anaongeza Cosmas.

Diwani wa Ndala, Zamda Shabani, anasema tatizo hilo wamelizungumza sana kwenye vikao vya Baraza la Madiwani, lakini hali bado ni mbaya na kuendelea kutaka halmashauri iwajibike.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, anasema uzembe wa uzoaji taka kwenye ghuba, ni tatizo la mji mzima wa manispaa hiyo, na kwamba kila mahali zimerundikana na uchafu kutishia afya za wananchi.

Anasema licha ya kujionea uchafu huo, pia amekuwa wakipigiwa simu sana na wananchi wakilalamikia hali hiyo kila wakati, na kubainisha kuwa kwa sasa wataweka utaratibu wa wazabuni kuanza kuzoa taka hizo na kuzipeleka dampo.

"Tunachokifanya kwa sasa ni kuona namna ya kuweka mzabuni wa kuanza kuzoa taka kwenye maghuba na kuzipeleka dampo, hali ambayo itamaliza kero hii na wananchi kuwa salama,"anasema Masumbuko.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Rajabu Masanche, anakiri tatizo la maghuba mengi kujaa uchafu, na kutolea ufafanuzi kuwa imesababishwa na ubovu wa magari ya kuzolea taka pamoja na mtambo wa kupakia takataka hizo kwenye magari ili kuzipeleka dampo.

Anasema watakachokifanya ni kukodi magari ili kuzoa taka kwenye vibanda na zitakuwa zikizolewa kwa awamu , wakati wakiendelea na matengenezo ya magari ya manispaa, ili zizolewe kila wakati na si mpaka yajae.

"Siyo kwamba manispaa tunapenda hali hiyo, bali ni changamoto za ubovu wa magari yetu ya kuzolewa taka, pamoja mtambo au kijiko na kuzipakia kwenye kijiko, ndiyo sababu kila mahali kumeelemewa na uchafu, lakini tutauzoa wote,"anasema Masanche.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anaziagiza halmashauri zote mkoani humo kuhakikisha wanaweka utaratibu maalumu wa uzoaji taka kwenye mabanda hayo , ili yasilete madhara kwa wananchi, pamoja vyumba hivyo kuwa visijengwe jirani na makazi ya watu, bali kwenye sehemu ambazo ni salama ili visihatarishe afya za wananchi.

## Walengwa TASAF vijijini wanapoibua vilio, vikwazo malipo kwa njia ya simu

**INATOKA UK.11**

Aidha, anasema kutokana na changamoto hiyo ya walengwa katika maeneo ya vijijini kutokuwa na simu, hawajui kusoma, na wala hakuna mawakala wa vibanda vya huduma ya kutoa pesa wataendelea na utaratibu wa kuwalipa malipo yao kwa njia ya awali.

Anatolea ufafanuzi pia fedha ambazo wanalipwa walengwa kwa mfumo huo wa simu na benki hazikatwi makato, sababu zinatumwa na makato yake ili mlengwa achukue pesa yake kamili, na kubainisha kuwa akitoa nusu nusu ndipo hela yake inakatwa.

Ofisa ufuatiliaji wa shughuli za TASAF wilayani na manispaa ya Shinyanga, Tabu Maro, anawataka walengwa ambao wapo karibu na huduma za kutoa pesa wasiishi kwa mazoea, bali wanunue simu ili waingizwe kwenye mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao ambao ni rahisi.

Pia walengwa wa TASAF wanahimizwa kutumia fedha kwa malengo yaliyokusudiwa, ili ziwatoe kwenye umaskini, na siyo kwenda kuzifanyia mambo ya anasa ikiwamo kuzinywea pombe na starehe nyingine.

Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga Zuwena Omary, akiwatetea wanaolalamikia kutokutambuliwa kwenye mfumo wa malipo, wanaosema vidole vyao havitambuliwi kwenye malipo kwa mfumo wa mtandao, anawataka waendelee kulipwa fedha zao.

Kwa wasio na Vitambulisho vya Taifa au NIDA licha ya kujaza fomu za maombi, ameiomba TASAF makao makuu kuwasiliana na mamlaka ya vitambulisho ili walengwa hao wapate vitambulisho hivyo na kuingizwa kwenye mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao.

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# LHRC, Wajapani wanapojitosa kuukabili unyanyasaji kingono

## • Klabu zaundwa kufikia walengwa



Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Christopher Newton, akielimisha wanafunzi kuhusu madhara ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono. **PICHA: SABATO KASIKA**

KATIKA juhudi za kuwanusuru wanafunzi na udhalilishaji, unyanyasaji wa kingono unaosababisha mimba kwa mabinti shuleni, wadau wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na walimu na wanafunzi wa shule za msingi, sekondari wa kata mbili za Dar es Salaam, wametangaza mkakati wa kuelimisha wanafunzi athari na njia za kudhibiti matendo hayo.

Wanufaika wa programu hiyo ni kata za Mwananyamala na Makumbusho ambazo wataanza na kuunda klabu katika shule za msingi Kinondoni, Msisiri A na B, Mwongozo na Kambangwa sekondari zilizoko kata ya Mwananyamala.

Shule za Msingi Minazini, Mwananyamala B, Mwananyamala Kisiwani, Mchangani, Makumbusho, Victoria na Sekondari ya Makumbusho iliyoko kwenye kata ya Makumbusho ni wanufaika wa mradi huo utakaosimamiwa na walimu wa malezi wa shule hizo.

Hayo yanaelezwa katika mwendelezo wa utambulisho wa mradi wa majaribio unaolenga kuzuia na kukabiliana na udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono kwa wanafunzi katika kata hizo unaofanyika hivi karibuni Dar es Salaam.

Ofisa Elimu wa Kata ya Mwanyalama, Joshua Biswalo, akizungumza kwenye utambulisho huo, anasema klabu hizo zitaundwa katika shule zote za msingi na za sekondari zikiwa na jukumu la kuwaelimisha wanafunzi kutambua mitego, vitendo na viashiria vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na kwamba zitakuwa zinakutana mara moja kwa wiki kutoa elimu.

"Walimu na wanafunzi walipata mafunzo ya jinsi ya kuepuka vitendo hivyo watakuwa kwenye klabu wakielimisha wanafunzi wenzao, chini ya usimamizi wa walimu wa malezi shuleni," anasema Biswalo.

Anataja suala jingine ambalo klabu hizo zitafanya, kuwa ni kuelezea athari za kisaikolojia ambazo mwanafunzi anakumbana nazo anapofanyiwa udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono utaratibu utakaotumiwa na shule za kata ya Makumbusho, kwa mujibu wa Ofisa Elimu wa kata hiyo, Simon Mirobo.

Anasema juhudi pia zinafanywa kuwabadilisha walimu kuwa marafiki wa wanafunzi na kuepuka ukali kupindukia ili wanafunzi wasiendelee kuwaogopa na wakidhalilishwa wafikishe taarifa kwao, tena wawe huru kuelezea changamoto wanazokutana nazo iwe nyumbani, njiani na hata shuleni ili kupunguza udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono.

> Manusura anaweza kuambukizwa maradhi ya kujamiiana ikiwamo virusi vya UKIMWI, kisonono, kaswende, homa ya ini, saratani na mlango wa kizazi pamoja na kupata mimba.

Christopher Newton kutoka Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto Mkoa wa Kinondoni, anapozungumza kuhusu mkakati huo anasema wanafunzi wakifahamu kuhusu vyanzo vya kuingizwa kwenye unyanyasaji huo watafahamu na kukwepa zawadi, lifti kwenye usafiri na kushikwa miili yao na wanaume kwa vile ni chanzo cha kutumbukia kwenye kudhalilishwa.

Anawakumbusha kuwa ni lazima wakatae na kufikisha taarifa kwenye Dawati la Jinsia na Watoto au Kituo cha Mkono kwa Mkono, ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria, kwa vile wakinyamaza, vitendo hivyo vitaendelea.

Mradi huo unafanywa na Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) na baadhi ya wadau kama Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto Mkoa wa Kinondoni.

Akizungumzia jukumu hilo wakili kutoka LHRC, Theresia Kinabo, anawataka wanafunzi kuwataja bila woga hata walimu ambao wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na vitendo hivyo vya unyanyasaji dhidi yao ili kuvikomesha.

"Tunasikia tuhuma za mara kwa mara kwamba wapo baadhi ya walimu wanaojihusisha na uhusiano na wanafunzi, hebu tumieni hizo klabu mtakazoanzisha ili kuwafichua," anasema.

### ZIPO ATHARI KISAIKOLOJIA

Mwanasaikolojia ambaye ni Mratibu wa Kituo cha Mkono kwa Mkono, Asia Mkini, anasema vitendo hivyo vinaweza kusababisha mwanafunzi kuathirika kisaikolojia na kujikuta akishuka katika masomo.

"Hivyo kuna haja ya kudhibiti udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, kwani umeshamiri kuanzia nyumbani, mitaani hadi shuleni, baadhi ya wanafunzi wanafanyiana mambo hayo wenyewe kwa wenyewe," anasema Asia.

Asia ambaye ni Ofisa Ustawi wa Jamii wa Kituo cha Mkono kwa Mkono, anasema, miongoni mwa kesi anazopokea kituoni hapo ni za wanafunzi kufanyiwa au kufanyiana vitendo hivyo.

"Wengine wanafanyiwa hawasemi kwa walimu wala kwa wazazi kwa kuwaogopa wanaowafanyia, katika mazingira hayo wanaathirika kisaikolojia kwa kuwa na msongo wa mawazo," anasema.

Anafafanua kuwa serikali imerahisisha kazi ya kuwasaidia manusura kwa kuanzisha vituo hivyo vyenye huduma mbalimbali sehemu moja zikiwamo za dawati la jinsia, madaktari, wanasheria na za ushauri nasaha.

### MADHARA KIAFYA

Dokta Lugano Msokwa anataja athari za unyanyasaji wa kingono ambazo klabu hizo zinapaswa kuwafundisha wanafunzi kuwa ni kujeruhiwa wanapofanyiwa kitendo cha kubakwa, hasa kwa watu wazima kutokana na kujitetea au michubuko sehemu za siri kwa watoto.

Anasema, manusura anaweza kuambukizwa maradhi ya kujamiiana ikiwamo virusi vya UKIMWI, kisonono, kaswende, homa ya ini, saratani na mlango wa kizazi pamoja na mimba.

"Kwa ujumla ni kwamba, vitendo hivyo ni hatari kwa afya iwe kwa wanafunzi wa kike hata wa kiume, kwani ninapokea kesi nyingi za watoto kulawitiwa na wengine kubakwa jambo ambalo ni hatari," anasema Dk. Lugano.

Anawataka wazazi na walezi kuwafuatilia watoto wao na pia kujenga urafiki na walimu, ili kupata taarifa mbalimbali za watoto wao, kwa madai kwamba matukio ya aina hiyo yanatokea pia katika mazingira ya shule.

SAYANSI
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Joto la nishati makaa ya mawe kuleta mwisho wa dunia



Makaa ya mawe na tanuru la kuyachakata ili kupata umeme. Vinu hivyo huzalisha hewa ukaa kwa wingi na kuongeza joto linalotishia hatima ya dunia na anga za juu. **PICHA: MTANDAO**

ONGEZEKO la joto duniani linalotokana na mabilioni ya tani za hewa ukaa (carbon) kujaa anga za juu, ni tatizo ambalo pamoja na kuongeza maafa, kuua watu na kuharibu mali, linaweza kuangamiza dunia kama sayari na viumbe wake, iwapo halitadhibitiwa.

Udhibiti unaotikisa mataifa yenye viwanda unaopendekezwa sasa ni wa kuachana na vyanzo vikuu vya nishati vinavyozalisha gesi ya ukaa, wakati wa kuvichakata ili kupata umeme.

Katika kukabiliana na gesi hiyo inayoweza kusababisha maangamizo, Umoja wa Mataifa (UN), unaagiza kukomesha uzalishaji wa nishati ya visukuu hasa makaa ya mawe, yanayotoa kaboni nyingi kupindukia.

Nishati za visukuku inatokana na mabaki ya wanyama na mimea yaliyofukiwa ardhini kwa karne nyingi na kutengeneza gesi au mafuta, inatajwa kuwa inazalisha hewa ukaa kwa wingi na kuchafua anga za juu na kuongeza joto duniani, ndiyo maana UN inapendekeza kuanza kutumia nishati jua, maji, upepo na hata nyuklia.

Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, anaziagiza serikali na sekta binafsi kuunda mtandao wa pamoja utakaofanikisha kuzisaidia nchi maskini kuachana na nishati hizo.

> “ Taarifa za ‘the U.S. Energy Information Administration’, zinasema chanzo kikuu cha nishati Marekani ni gasi asilia, makaa ya mawe na nyukilia.

Kwa mujibu wa Guterres, kipaumbele cha kwanza ni kuondokana na vyanzo vya nishati za visukuku hasa makaa ya mawe kwa awamu, akisema hakuna tena kujenga mitambo ya kuzalisha umeme wa makaa hayo.

Anayasema hayo, akihutubia mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) kwa njia ya mtandao kutokana na kuwapo COVID-19 na kuwaeleza viongozi wa sekta ya biashara wanaoshiriki kwenye jukwaa hilo kuwa kinachokosekana hivi sasa duniani ni mshikamano wa kimataifa.

Anasema ni jambo la dharura na ni hatua ya kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kutishia hatima ya dunia.

Anaziambia nchi zinazoendelea kuwa kama zitatekeleza ahadi zao za kupunguza utoaji hewa chafuzi ifikapo mwaka 2030, utoaji wa hewa chafu duniani bado utasalia kuwa mkubwa na kwamba ni lazima kudhibiti kiwango cha joto kisizidi nyuzi joto 1.5.

Katibu Mkuu anasema ongezeko la nyuzi joto 1.2 tayari limeleta madhara makubwa na wengi wameshuhudia.

Anasema mwaka jana hali ya hewa mbaya kupita kiasi imesababisha vifo vya watu zaidi ya 10,000 na hasara dola bilioni 120 (takribani Shilingi trilioni 300).

Mwaka 2020 majanga ya tabianchi yamesababisha watu milioni 30 kukimbia makazi yao, idadi ambayo ni mara tatu zaidi ya wale waliolazimika kukimbia makazi yao kutokana na vita na ghasia.

“Kurekebisha mwelekeo kunahitaji utashi wa dhati kutoka kwa serikali na sekta ya biashara katika kila nchi ambayo inatoa hewa zinazochafua dunia.” Anasema Guterres.

Anasema katika maeneo hayo jamii ya kimataifa inahitaji kuungwa mkono, kupata mawazo, fedha na sauti ya jamii ya wafanyabiashara duniani.

### WACHAFUZI WAKUU

Mchafuzi wa kwanza duniani kwa kutoa kiwango kikubwa cha hewa ukaa ni China inayozalisha zaidi ya tani bilioni 10.67 ya gesi hiyo, kiwango kilichorekodiwa mwaka 2020 na kuifanya kushika nafasi ya juu kwa kuchangia mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la joto zaidi duniani.

Kwa mujibu wa ‘Science for a Changing World’, Marekani ilizalisha tani bilioni 5.1 za hewa ya kaboni (ukaa) mwaka 2019, wakati dunia nzima kiasi cha tani bilioni 33.1 kilizalishwa.

Mtandao wa ‘Climate Trade’, unataja mataifa mengine wazalishaji wakuu kuwa ni India inayozalisha tani bilioni 3.0, Russia tani bilioni 1.7, inafuatiwa na Japan inayotoa tani bilioni 1.6, Ujerumani tani milioni 759, wakati Iran nayo ni moja ya mataifa ya 10 bora kwenye uzalishaji wa hewa ukaa yenye tani milioni 720.

Korea Kusini imo kwenye kundi hilio kwa kuzalisha tani 659 milioni, Saudia Arabia inazalisha tani milioni 621, Indonesia tani milioni 615 ni kwa mujibu wa Climate Trade.

Afrika Kusini ni ya kwanza barani Afrika ikichangia uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuzalisha tani milioni 479 za hewa ukaa.

Kwa Tanzania mwaka 2020 kaboni iliyozalishwa ilifikia tani milioni 11.5, kwa mujibu wa taarifa ‘World DataAtlas’.

Guterres anasema mkutano wa mwaka huu wa jukwaa la biashara-WEF unafanyika kukiwa na changamoto kubwa zinazoukumba uchumi wa dunia, wakazi wake na dunia yenyewe kama sayari.

Katika uchafuzi wa hali ya hewa China inatajwa kuwa pekee inazalisha carbon nyingi ikilinganishwa na mataifa yaliyoendelea na hata kiasi kinachozalishwa kikichangnywa.

Hata hivyo ongezeko la uzalishaji wa gesi hiyo utabakia kuwa kitisho mpaka Marekani na China zitakapokubaliana namna bora ya kupunguza uzalishaji.

China ni mtumiaji namba moja wa nishati ya makaa ya mawe ikizalishaji gigawati milioni 4.5, kama asilimia 62.2 ya nishati yake, aidha inatumia gesi asilia kuzalisha nishati gigawati 232,500, pia hutumia joto ardhi.

Taarifa za ‘the U.S. Energy Information Administration’, zinasema chanzo kikuu cha nishati Marekani ni gasi asilia, makaa ya mawe na nyukilia. Nchini India, chanzo kikubwa ni makaa ya mawe, mafuta mazito, gesi asilia, joto ardhi pamoja na miti.

Kutumia makaa ya mawe kunaelezwa kuwa ni hatari kwa usalama wa dunia hasa kutokana na kuongeza joto kali kwa vile makaa hayo yakiunguzwa ili kupata nishati yanatoa kiwango kikubwa cha hewa ukaa ambayo inapofika angani inatandaa na kusambaa kama blanketi, lakini ikiwa na joto jingi na kuendelea kulihifadhi kwa miongo kadhaa.

Joto hilo kama blanketi huachilia joto linalorudi duniani na kusababisha fukuto ambalo linahatarisha usalama wa viumbe hai, dunia yenyewe na mfumo mzima wa mazingira.



## Mkakati waja na kasi ya upasuaji mabusha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema inaweka mipango sawa ili kuhakikisha angalau wagonjwa 60 wa mabusha wanafanyiwa upasuaji kwa siku kupunguza idadi ya watu wenye ugonjwa.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Afya, Godwin Mollel, wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele kama mabusha na matende, kichocho, usubi, na trakoma.

Alisema kwa kuwa serikali imeziwezesha hospitali zote za mikoa kambi maalum zinaweza kuandaliwa kwa ajili ya kupeleka wataalamu kwenye maeneo ya tatizo hilo ili kuharakisha upasuaji kwa watu wenye shida ya mabusha ambao wanakadiriwa kufikia 29,500.

Alisema kasi ambayo mpango wa taifa wa kudhibiti magonjwa hayo inaenda nayo ni ndogo na iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa inaweza kuchukua miaka mingi kuwafikia wananchi wenye shida hiyo kwa kuwa takwimu zilizoko zinaonyesha kuwa ni watu 8,191 tu waliofanyiwa upasuaji mpaka kufikia mwaka jana.

"Sijaagiza mkafanye hivyo ila ni jambo ambalo tukijipanga linatekelezeka. Njooni ofisini kwangu tukae tuone kama inawezekana tufanye hivyo na mimi naamini kabisa inawezekana kwa sababu kumfanyia upasuaji mgonjwa wa mabusha hakuhitaji ubobezi sana," alisema Mollel.

Kwa mujibu wa takwimu zilizoko kwa mwaka watu wasiozidi 1,200 ndio wamekuwa wakifanyiwa upasuaji wa mabusha kwa mwaka ambao ni wastani wa watu wanne kwa siku kasi ambayo waziri alishauri iongezwe mpaka kufikia upasuaji wa watu 60 kwa siku.

Meneja Mpango huo, Dk. George Kabona, alisema kwa sasa gharama ya upasuaji wa mabusha kwa mtu mmoja inakadiriwa kufikia Sh. 250,000 na mpaka kufikia mwaka 2021 mpango huo umeshawafanyia upasuaji watu 8,191 na nchi nzima inakadiriwa kuwa na wagonjwa 29,500 wenye mabusha.

Alisema mwaka 2008, mpango huo ulifanikiwa kuwafanyia upasuaji wagonjwa 200, mwaka 2013 wagonjwa 680, mwaka 2015 wagonjwa 315, mwaka 2016 wagonjwa 709 na mwaka 2017 wagonjwa 1,239 wakati mwaka 2018 walifanyiwa wagonjwa 1,441.

Dk. Kabona alisema mwaka 2019 mpango huo ulifanikiwa kuwafanyia upasuaji watu 1,387, mwaka 2020 watu 1,054 wakati mwaka 2021 walifanya upasuaji kwa watu 1,116 na kwamba mpango huo ulizinduliwa mwaka 2009 kwa ushirikiano na Shirika la Kudhibiti Usubi Afrika na Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID).

# Wasaidizi wa sheria ngazi ya cheti kunolewa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya wasaidizi wa kisheria ngazi ya cheti.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo kwenye maonyesho ya Wiki ya Sheria, Ofisa Habari, Elimu na Mawasiliano kutoka taasisi hiyo, Scholastica Njozi, alisema mafunzo hayo yataanza kutolewa Septemba mwaka huu ikiwa ni baada ya kupata ithibati na usajili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ( NACTE).

Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 pamoja na mambo mengine, inaelekeza kuwa mafunzo ya wasaidizi wa kisheria yatatolewa katika ngazi mbalimbali na kwa kufuata utaratibu ulioainishwa ndani ya sheria ambapo ngazi za mafunzo zitakuwa ni mafunzo ya muda mfupi miezi mitatu mpaka sita, mafunzo ya ngazi ya cheti na mafunzo ngazi ya diploma.

Njozi alisema sifa za kujiunga na mafunzo hayo ni mtu yeyote aliyehitimu elimu ya kidato cha nne na kuendelea na mwenye ufaulu wa alama D kwenye masomo manne ya kidato cha nne ikiwamo somo la Kiingereza.

Alisema mafunzo ya wasaidizi wa kisheria ngazi ya cheti yatatolewa kwa muda wa mwaka mmoja na yatatolewa kwa nadharia na vitendo.

"Tunawakaribisha Watanzania wenye sifa kuja kujiunga pindi utakapofungua dirisha za udahili na mafunzo yatatolewa kwa mwaka mmoja ambapo miezi mitano wanafunzi watajifunza wakiwa darasani na miezi mingine mitano watajifunza wakiwa sehemu za kazi kwenye taasisi zinazotoa msaada wa kisheria.

"Taasisi inajivunia kuwa ndio taasisi ya kwanza kutoa mafunzi haya kwa ngazi ya cheti." Aidha, Njozi alisema pia taasisi ipo kwenye mchakato wa kuandaa mtaala wa diploma ambapo wanafunzi watakapomaliza mafunzo ngazi ya cheti ataweza kuendelea mbele kwa ngazi ya diploma.

"Mafunzo yatakayotolewa yatakuwa na ubora ambao utamwezesha mwanafunzi kufanya kazi kama msaidizi kisheria au kuendelea mbele kimasomo ngazi ya diploma au shahada iwapo mtapenda kufanya hiyo kitakachotolewa kitakuwa kinatambuliwa na NACTE."



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (katikati), akiangalia moja ya vifaa vya kisasa vilivyonunuliwa na Halmashauri ya Jiji kwa Sh. milioni 240 kwa ajili ya upimaji wa viwanja kwenye uzinduzi uliofanyika juzi, (kushoto) Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru na Mstahiki Meya wa Jiji, Devid Mwamfupe (wapili kulia). **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jiji laachana na kampuni binafsi upimaji wa ardhi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amesema kuwa kupatikana kwa vifaa vipya vya kisasa vya upimaji ardhi kwenye halmashauri hiyo, kuanzia sasa hawataingia tena mikataba na kampuni binafsi ya upimaji.

Mafuru alisema hayo wakati wa kuzindua vifaa hivyo vya kisasa vilivyonunuliwa kwa gharama ya Sh. milioni 240. kwa fedha za mapato ya ndani ya Jiji.

Alisema baada ya Jiji kupata vifaa vyake gharama za upimaji itakuwa Sh. 120,000 ambapo awali gharama za upimaji kwa kampuni binafsi za upimaji ni Sh. 250,000.

Alisema kuwa upatikanaji wa vifaa hivyo ni mategemeo yao sasa kutoingia nao mikataba na kampuni binafsi za upimaji na zzitakazoendelea na kazi hiyo baada ya kazi zao kumalizia itakuwa imekwisha.

Alisema kuwa kampuni binafsi zimekuwa zikilalamikiwa na kusababisha migogoro mingi ya ardhi ilikuwa inatengenezwa na kulalamikiwa halmashauri ya jiji.

Alisema kuwa viwanja vilikuwa vinagawanywa ni vidogo vidogo, ili kuongeza faida na kwenye maeneo mengi kulikuwa kunaibuka migogoro kila siku.

Alisema awali Jiji lilikuwa na mahitaji makubwa ya upimaji viwanja na isingeweza kufanya kazi hiyo peke yake ndipo wakaalika kampuni binafsi, lakini mwisho wa siku walizalisha migogoro mingi na kunyoshewa vidole vya kuilalamikia.

Alisema walikuwa na mikakati mingi ya kuimarisha shughuli za upimaji ardhi na mwaka 2019 walinunua magari matatu na mwaka 2020 walinunua tena magari matatu.

Alisema lengo ni kupima viwanja 300 kwa siku na watakwenda kupima maeneo ambayo upimaji ulisimama kwenye maeneo mbalimbali ndani ya halmashauri hiyo.

Alitaja maeneo hayo ni Bihawana, Gawaye, Hombolo na maeneo ya pembezoni ambayo upimaji ulisimama na upimaji huo utafanyika kwa gharama nafuu.

Alisema sasa wanakwenda kununua magari na mitambo kwa ajili ya kufungua barabara ili kufanya Dodoma kuwa Mji uliopangwa kuliko miji yote.

"Tunaenda kufungua barabara na kufanya mapinduzi makubwa kwenye sekta ya ardhi," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jabir Shekimweri, alisema vifaa hivyo kama vitatumika vizuri vitapunguza changamoto ya upimaji katika maeneo mengi.

Alisema wakati Jiji linakabidhiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) wakati wanakabidhiwa kutoka CDA kulikuwa na mahitaji ya viwanja 20,000 lakini kazi kubwa ilifanyika.

"Jiji kupata seti sita zenye uwezo wa kupima viwanja 300 kwa siku sawa na viwanja 9,000 kwa mwezi ni jambo la kupongezwa," alisema.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji Jiji la Dodoma, Amelye Chaula, akitoa taarifa ya upatikanaji wa vifaa hivyo, alisema kuwa hivi sasa itawaondolea gharama ya kulipia kampuni ambazo ilikuwa ikiongezeka kila wakati.

Pia itaondoa malalamiko kutoka kwa wananchi yanayotokana na upimaji wa kampuni ambazo zilikuwa zikipima viwanja vidogo vidogo ili kuongezea faida.



# 3,000 kupewa mbegu za majaribio za maharage

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya wakulima 3,000 nchini, wanatarajiwa kupatiwa mbegu mpya za maharage za majaribio ili kupima ubora na uzalishaji wa mbegu hizo kabla ya kuanza kusambazwa kwa wakulima wengine.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema matokeo hayo ni jitihada za watafiti wa mazao ya chakula na biashara kutoka TARI ambao wamejikita kuwasaidia wakulima ili kupata mavuno mengi.

Dk. Bucheyeki alisema wameanzisha mpango wa kutafiti mbegu mpya za mazao mbalimbali zitazohimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Uamuzi wa kuwapatia wakulima mbegu mpya za maharage uliafikiwa baada ya kufanyika kikao cha wadau wa kilimo kutoka mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Mbeya, Rukwa, Songwe na Ruvuma ambapo walikubaliana kufanya tathmini ya mbegu mpya za maharage na mazao mengine ambayo yameanza kufanyiwa utafiti kabla ya kuanza kuyasambaza kwa wakulima.

"Wataalamu wamekuja na ubunifu huo wa mbegu mpya ili kuwasaidia wakulima kukabiliana na changamoto zilizoko mpango huo unalenga kuwafikia wakulima zaidi ya 3,000 nchi zima ambao watafanyiwa majaribio ya awali kabla ya kuanza kuisambazwa kwa wakulima wengine," alisema Dk. Bucheyeki.

Mtafiti wa zao la maharage kutoka Tari Uyole, Catherine Mwakabungu, alisema mbegu hizo mpya za maharage zimebuniwa kwa kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema mbegu hizi zitaweza kuhimili hali ya hewa mahali popote na kwamba kila mwaka wakulima 1,000 wataweza kunufaika na mbegu hizo ambazo alisema zina mavuno mengi.

Miongoni mwa wadau uzalishaji mbegu Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Fadhili Kasubiri, alisema mbegu hizi zimekuja wakati muafaka na zitawasaidia wakulima kujikwamua na umaskini kwa kupata mavuno mengi.

Msindikaji wa mazao, kutoka eneo la Ikowo mkoani Rukwa, Remi Mariva, alisema kwa kipindi kirefu wamepata mavuno kidogo kutokana na aina ya mbegu wanazozitumia.

Alisema anaamini mbegu hizo mpya za maharage zitasaidia kupata mavuno mengi na kurahisisha shughuli za kusindika mazao.



Baadhi ya mafundi wasaidizi wanaojenga barabara ya Roma- Kalumbulu iliyoko katikati ya Mji wa Kyela mkoani Mbeya, wakiendelea na shughuli za kuchanganya mchanga juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wahudumu wa afya wahimizwa matumizi sahihi dawa vifaa tiba

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAIMU Meneja wa Mamlaka ya Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi (TMDA) mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, amewakumbusha wahudumu wa vituo vya afya na zahanati kuzingatia matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa kuhakikisha hawatumii dawa zilizokwisha muda wake.

Mshighati alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika kikao cha Kamati ya Ushauri cha Mkoa (RCC) wakati akiwakilisha utekelezaji wa mamlaka hiyo kwa mwaka 2021/2022, na kusema hatua hiyo ni kuepusha kuhatarisha afya ya wananchi.

Aliwakumbusha wahudumu na wataalamu wa afya kuzingatia matumizi ya dawa na vifaa tiba katika maeneo yao kwa kuhakikisha wanazingatia ubora na ukomo wa matumizi kabla ya kuwapatia wagonjwa wanaofika kwa ajili ya kupata matibabu.

"Katika ukaguzi wetu hadi sasa tumebaini asilimia 46 ya dawa zilizopigwa marufuku katika maeneo mbalimbali ikiwamo maduka na vituo vya afya vilevile tulibaini asilimia 19 ya dawa zinazouzwa zimekwisha muda wake, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi na wataalamu wa afya kuzingatia ubora na ukomo wa dawa ili kulinda afya za watumiaji," alisema Mshighati.

Aidha, alieleza kuwa wanaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara pamoja na doria kwenye mipaka na maeneo yanayohisiwa kutumika kuingia magendo na kutoa tahadhari kwamba wanaobainika wanaendelea kuchukuliwa hatua ikiwamo kufikishwa mahakamani na kutaifishwa bidhaa zao.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliwaomba wataalamu pamoja na wahudumu wa afya kushirikiana na TMDA kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na matumizi ya dawa zinazohitajika ili kulinda afya za wananchi.

# Milioni 500 kukamilisha mradi wa maji Chunya

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI imetoa shilingi milioni 507 kwa ajili ya kukamilisha mradi mkubwa wa maji katika Kata ya Sangambi wilayani Chunya.

Mradi huo unatajwa kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji katika eneo hilo na kuhudumia maeneo yanayozunguka kata hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mbunge wa Jimbo la Lupa lililoko wilayani Chunya, Masache Kasaka, alisema tayari serikali imeingiza fedha yote shilingi milioni 507 ambazo zinahitajika kukamilisha mradi huo wa maji.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Chunya wanapata maji ya uhakika serikali kupitia Wizara ya Maji imeanza usanifu wa kutafuta chanzo cha uhakika cha maji kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa eneo la Chunya Mjini. Alisema hadi sasa upatikanaji wa maji katika wilaya hiyo ni kwa asilimia 30, na kwamba kwa kushirikiana na serikali wanaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali na fedha ili kukamilisha miradi ya maji inayojengwa na inayotarajiwa kujengwa.

"Wilaya yetu inapata maji kwa asilimia 30, hii ni kutokana na jiografia ya eneo hili kuwa kame, lakini kukosekana kwa vyanzo vingi vya maji serikali imejitahidi kujenga miradi ya maji katika baadhi ya maeneo, lakini bado tatizo lipo tunachokifanya kwa sasa ni wataalamu ambao ni Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kuendelea kufanya utafiti kubaini vyanzo vingi vya maji ili vianze kujengwa," alisema Masache.

Aliongeza kuwa miongoni mwa mafanikio katika kuhakikisha huduma ya maji inaboreshwa ni kukamilika kwa mradi wa Matwiga ambao umekamilika kwa asilimia 100.

Alisema mradi huo utaanza kutoa maji mapema mwezi Februari ambapo wakazi wa maeneo mbalimbali watanufaika wakiwamo wa Makongolosi na Matundasi. Baadhi ya wananchi wa eneo hilo wameishukuru serikali kwa kuendelea kuwasogezea karibu huduma ya maji na kwamba awali walikuwa wakitumia umbali mrefu kufuata maji ya visima kwa wawekezaji wa migodi ya dhahabu.

Raphael Abdallah, alisema wakati mwingine wanalazimika kuchangia maji na wanyama kwenye mito ambayo yalikuwa sio safi na salama kwa matumizi ya binadamu.



# Rais Mwinyi awaapisha watendaji wapya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaapisha watendaji mbalimbali aliowateua hivi karibuni kushika nyadhifa zao.

Hafla hiyo ya kiapo imefanyika jana Ikulu, jijini Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi wakuu wa kitaifa, mawaziri, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini pamoja na wanafamilia.

Viongozi walioapishwa kushika nyadhifa hizo ni pamoja na Jaji Aziza Iddi Sued aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani ya Idara Maalum za SMZ pamoja na Dk. Said Seif Mzee kuwa Mhasibu Mkuu wa Serikali Zanzibar katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Mwingine ni Dk. Rahma Salim Mahafoudh aliyeteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria hafla hiyo ni pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmeid Said, Mufti Mkuu wa Zanzibar Shekhe Saleh Omar Kaab, mawaziri, wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama, viongozi wa vyama vya siasa pamoja na wanafamilia.

**Hafla hiyo ya kiapo imefanyika jana Ikulu, jijini Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi wakuu wa kitaifa, mawaziri, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini pamoja na wanafamilia.**

# DC kufuatilia utekelezaji miradi ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa, amesema atafuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mkoa huo ili itekelezwe kwa muda uliopangwa na kiwango kinachotakiwa.

Aliyasema hayo wakati akifungua kikao cha kamati ya maendeleo ya mkoa huo kilichofanyika katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Mjini Zanzibar.

Alisema hatosita kuishauri serikali kuu kuhusu mkandarasi yeyote atakayebainika kuchelewesha ujenzi ama kujenga chini ya kiwango.

Alisema mipango ya serikali haitafanikiwa ikiwa baadhi ya watu wasio na nia njema wanashindwa kutimiza wajibu wao ama kufanya hujuma.

"Niwaombe waheshimiwa wabunge, wawakilishi na viongozi wa wilaya na manispaa tuwe tunafanya ziara za mara kwa mara kukagua miradi inayotekelezwa katika maeneo yetu ili kuona namna inavyoendelea," alisema Kitwana.

Akizungumzia usafi wa mji, Mkuu wa Mkoa huyo alisema bado hajaridhishwa na hali ya usafi wa mji hasa katika barabara kuu na kuyataka mabaraza ya Manispaa kuchukua juhudi za kuzisafisha barabara kuu, masoko na maeneo mengine yanayotoa huduma za kijamii.

Alisema vitendo vya udhalilishaji hasa kwa watoto vimekuwa vikiongezeka licha ya juhudi kubwa zinazoendelea kuchukuliwa na serikali.

"Wanaoathirika zaidi ni watoto wetu ambao ndiyo tegemeo la taifa letu la kesho... kama viongozi tuna wajibu wa kuona matendo ya udhalilishaji tunayadhibiti na yanamalizika katika mkoa wetu," alisema.

Akizungumzia kuhusu hali ya amali na usalama ya mkoa huo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Abdallah Hussein Mussa, alisema kuwa hali ya uhalifu katika mkoa huo umepungua kutokana na ongezeko la misako na doria na utoaji wa elimu kwa raia.

Alisema katika kudhibiti vitendo vya udhalilishaji na matumizi ya dawa za kulevya wamejiwekea mikakati mbalimbali ikiwamo kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kwa muda mfupi na kutotoa dhamana kwa watuhumiwa wa kesi za udhalilishaji.

Kamanda huyo alisema kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka jana, kulikuwa na makosa 231 dhidi ya binadamu ikiwamo mauaji, ubakaji na mengine, makosa ya unyang'anyi wa mali ikiwamo wizi yalikuwa 189 kwa kipindi hicho na makosa dhidi ya maadili ikiwamo dawa za kulevya 135.

"Makosa ya udhalilishaji pekee kwa kipindi cha mwezi wa Julai hadi Desemba mwaka jana katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja ni kuingilia kinyume na maumbile (19), kubaka (150), kulawiti (45), kunajisi (14)," alisema.



Viongozi wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama Zanzibar waliohudhuria hafla ya kuapishwa walioteuliwa na Rais kushika nafasi mbalimbali katika ukumbi wa Ikulu jijini Zanzibar, jana. **PICHA: IKULU**

# Zanzibar yapokea dozi 200,000 chanjo UVIKO-19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imepokea dozi 200,000 za chanjo ya UVIKO-19 aina ya Sinopharm kutoka China ambazo zitatumika kuchanja wananchi 100,000.

Akipokea dozi hizo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kutoka kwa Ubalozi wa China, Kaimu Waziri wa Afya, Simai Muhammed Said, aliipongeza Serikali ya China kwa kuwezesha upatikanaji wa chanjo hizo.

"Hii ni awamu ya pili kwa chanjo za aina hii kutoka Serikali ya China kupatikana hapa Zanzibar. Awamu ya kwanza tulipokea jumla ya dozi 110,000 za chanjo aina ya Sinovac, ambazo zilitumika kuchanja wananchi 52,000," alisema.

Waziri Simai alisema, mapokezi ya chanjo hizo yanafanya jumla ya chanjo zilizopokelewa tangu Zanzibar kutoa chanjo dhidi ya UVIKO-19 hadi sasa ni dozi 422,520 zikijumuisha chanjo za (Sinopharm, Jenssen, Sputnik Light, Sinovac na Pfizer), ambazo zinatosha kuchanja jumla ya wananchi 240,000.

Alisema kuwa hadi kufikia Januari 21, mwaka huu, watu 139,431 wamepata chanjo na kati ya hao waliopata hakuna taarifa ya madhara yoyote zaidi ya maudhi madogo yaliyosababishwa na chanjo hizo.

Alisema chanjo hizo ni muhimu kwa wananchi na zipo salama na zimethibitika kuongeza kinga ya mwili na kupunguza makali ya ugonjwa wa UVIKO-19 kwa wale wanaopata maambukizi ya virusi hivyo.

Simai ambaye ni Waziri wa Elimu na mafunzo ya amali alisema, takwimu zinaonyesha kuwa mikoa inayofanya vizuri katika kutekeleza utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 ni wa Mjini Magharibi na hasa Wilaya ya Mjini, kwa asilimia 22, Mkoa wa Kusini Pemba asilimia 16 na Mkoa wa Kaskazini Pemba asilimia 12.

"Kadhalika mikoa ya Kusini Unguja na Kaskazini Unguja kunahitajika jitihada za ziada katika kupata chanjo hizo hasa katika Wilaya ya Kati Unguja na Kaskazini A," alisema.

Alisema katika kufikia kinga jamii dhidi ya UVIKO-19, serikali inalenga kuchanja wastani wa asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu na kuwataka wakuu wa mikoa kuongeza juhudi za uhamasishaji jamii ili kuongeza kiwango cha utoaji wa chanjo na kuhimiza wananchi wakapate chanjo kama inavyoshauriwa na wataalamu.

Kwa upande wake Balozi mdogo wa China aliyopo Zanzibar, Zhan Zhisheng alisema, China daima itasimama pamoja na Zanzibar katika mapambano dhidi ya janga hilo la corona na China itaendelea kubadilishana uzoefu na kutoa misaada kulingana na uwezo wao.

"Ulimwengu unashuhudia mabadiliko makubwa ambayo hayajaonekana kwa miaka mia moja. Mlipuko wa Covid-19 huleta changamoto kubwa kwa wanadamu," alisema Balozi huyo akimnukuu Rais wa China, Xi Jinping.

Alisema tayari China imetuma zaidi ya dozi bilioni mbili za chanjo kwa zaidi ya nchi 120 na mashirika ya kimataifa pia itatoa dozi zingine bilioni moja kwa nchi za Afrika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**UMMI SHOMARI MUKHANDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1200/0049 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya EDUCARE mwaka 2012,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/URA/RB/44898/202**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**VICTOR BETRAM MCHUNGWA** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba TAE 318603 iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi mwaka 2021,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DOD/DOD/RB/37189/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**STEVEN EDWARD MJENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TRAILER yenye namba za usajili T 400 AVE, na kadi ya gari aina ya HORSE yenye namba za usajili T 325 BBR,yeyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MKB/RB/358/2022**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY)**
**(ONE STOP JUDICAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**
**In the matter of the estate of the late**
**Paul Frederick Gatrell..................Deceased**
**And**
**In the matter of an application for sealing of the letters of administration**
**By**
**Helen De Vere Van Der Linden............1st Application**
**Clare Lina Pitman..........................2nd Application**
**NOTICE OF APPLICATION FOR RESEALING**
**(Rule 99)**

Notice is hereby given that an application has been made to this Court for sealing of the letters of administration of the estate of Paul Frederick Gatrell, late of Malawi, who died at Blantyre Adventist Hospital in Malawi on the 15th day of September 2017, granted to Helen De Vere Van Der Linden and Claire Lina Pitman, of Malawi by the High Court of Malawi and that the said application will be heard at this Court by a Judge in Chambers on the **14th day of February, 2022 at 9:00 O'clock in the morning.**
**Dated at Dar es salaam, this 1st day of December, 2021.**

HIGH COURT OF TANZANIA

Deputy Registrar

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KILOSA**
**WILAYA YA KILOSA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 47 YA 2021**
**(Linatoka na Kesi ya Madai Na.9/2020 kutoka Mahakama ya Mwanzo Magole)**
**MUOMBAJI: MOLEN ROBISON MWAGILE**
**DHIDI YA**
**MJIBU MAOMBI: DANIEL EDWARD SHIJA**

**YAH; KUITWA SHAURINI POPOTE PALE ULIPO**

Fahamu kwamba mdai ameleta maombi madogo dhidi yako.Maombi hayo madogo yamepangwa kusikilizwa Tarehe 25/02/2022.Fahamu kwamba unatakiwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe/Wakili wako siku hiyo bila kukosa.Kutokuhudhuria kwako kutaifanya mahakama hii iendelee na shauri hili bila kuwepo na kulitolea maamuzi.
**Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 mwezi 01 mwaka 2022.**

.......................................................
HAKIMU MKAZI WA MAHAKAMA YA WILAYA KILOSA

## TANGAZO!!
### AFRIWELD INDUSTRIES LTD
### Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35
**Nafasi:** Mauzo
MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!!
wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!
Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**
Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni
**01/01/2022 MPAKA 15/02/2022**
**Asante**
116653602

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. M
OB: +255 - 0782253676

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Serikali yaunda kamati kudhibiti mauaji nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeunda kamati itakayokuja na mkakati wa kitaifa utakaotoa suluhu ya kudumu ya kudhibiti matukio ya mauaji ya watu kikatili ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara katika maeneo mbalimbali.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu kikao cha viongozi wakuu wa wizara hiyo na Jeshi la Polisi kilichokutana kwa lengo la kujadili matukio ya mauaji nchini.

Masauni, alisema kamati hiyo ameipa muda wa siku 21, kuishauri serikali na kuja na mkakati wa kitaifa kudhibiti matukio hayo ya mauaji nchini.

Alisema katika kipindi cha mwezi mmoja wa Januari mwaka huu jumla ya matukio ya mauaji 179 yameripotiwa na zaidi ya watu 150 waliohusika wamekatwa na Jeshi la Polisi.

Alisema, kutokana na kukithiri kwa matukio hayo nchini kikao hicho kimelazimika kuunda kamati ambayo itakuwa na jukumu la kuandaa mkakati wa kitaifa wa kupata suluhu ya kudumu ya matukio hayo.

Kadhalika alisema kamati hiyo itaundwa na wataalamu mbalimbali kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Wakili mkuu wa serikali, Idara ya Usalama wa Taifa, Ustawi wa Jamii.

Wataalamu wengi ni kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), TAKUKURU, Taasisi ya Elimu ya Juu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali, Wizara ya Habari na Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

"Katika kipindi hicho cha siku 21 ningependa kamati hii kuanza na mikoa ambayo imeonekana kuongoza katika matukio haya ya mauaji katika kipindi hicho cha mwezi mmoja ukiwamo mkoa wa Kagera, Dodoma, Tabora, Kigoma, na Songwe," alisisitiza Masauni.

Pia alifungua milango kwa mtu yeyote ambaye ataona anaouwezo wa kushirikiana na kamati hiyo kusaidia kuja na mawazo ambayo yatasaidia kudhibiti matukio hayo ya mauaji nchini.

Mbali na kuundwa kwa kamati hiyo Masauni alitoa maagizo kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa watu wote ambao wamehusika na matukio ya mauaji ya aina yoyote ile kukamatwa na sheria kuchukua mkondo wake.

"Mbali na maelekezo ya Mkamu wa Rais aliyoyatoa hivi karibu, mimi pia natumia fursa hii kuliagiza Jeshi la Polisi nchini kuhakikisha kuwa kila aliyehusika na mauaji ya aina yoyote ile anakamatwa na kufikishwa katika mkono wa sharia," alisema.

Alisema kazi ya kuwakamata watuhumiwa wa mauaji si kazi ya Jeshi la Polisi peke yake bali kila mtu anao wajibu wa kutoa ushirikiano ili iwe rahisi kuwapata wahusika.

"Matukio mengi ya mauaji yamekuwa yakisababishwa na migogoro ya kifamilia kama vile mirathi, migogoro ya ardhi, ulevi, visasi, chuki na ushirikina vitu ambavyo vinatakiwa kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu," alisisitiza Masauni.

Hata hivyo, alisema kuhusu tukio la mauaji lilitokea jijini Dodoma na watu watano wa familia moja kuuawa ndani ya nyumba yao taarifa yake wanatarajia kufikisha kwa Makamu wa Rais ndani ya siku mbili zijazo.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi Benki ya NMB, Aikansia Muro, akibonyeza kitufe cha kompyuta kumtafuta mshindi wa droo ya mwezi ya kampeni ya 'NMB MastaBata Kivyako Vyako' iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkaguzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Pendo Mfuru na Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sita wauawa mapigano ya wakulima, wafugaji

**Na Hamida Kamchalla,**

KILINDI

WATU sita wameuawa katika mapigano ya wakulima na wafugaji kwenye vijiji viwili mikoa ya Tanga na Manyara.

Hadi kufikia jana mchana, watu sita walikuwa wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa vibaya kwa silaha za jadi katika kijiji cha Kibirashi kilichoko Wilaya ya Kilindi (Tanga) na Kijiji cha Elerai Wilaya ya Kiteto (Manyara).

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, chanzo cha mauaji hayo ni wafugaji wa Kijiji cha Elerai kuvamia Kijiji cha Kibirishi na kuanza kuwashambulia wakulima kwa risasi na baadaye kutumia mapanga.

Alisema watu hao waligundulika kuuawa na miili yao kutelekezwa, Januari 30 mwaka huu.

"Ni kweli hayo mauaji yametokea. Kuna familia moja ya wafugaji wakiwa ndani ya boma, walivamiwa na kijana wa miaka 25, walimpiga risasi tumboni na begani.

"Baada ya tukio hilo, pakazuka taharuki kwa jamii ya wafugaji, wakidhani wamevamiwa kutokana na mgogoro wao ulioko na Kijiji cha Kibirashi.

"Kutokana na hali hiyo, yakaanza matukio yaliyosababisha wafugaji wa kuua wakulima watatu, lakini wakulima nao, wakaanza kushambulia wakawaua wafugaji watatu. Kwa hiyo waliofariki ni sita hadi sasa."

Kwa mujibu wa kamanda huyo, waliopoteza maisha ni mwanamke mmoja, wavulana wanne na mtoto wa miaka saba.

Kutokana na mauaji hayo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, alisema waliotekeleza mauaji hayo watakamatwa wakiwa hai au wafu.

## Gwajima, Silaa wamaliza 'kifungo' cha Bunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE waliokuwa wanatumikia adhabu ya kitohudhuria mikutano miwili ya Bunge, wanatarajia kuhudhuria baada ya kumaliza adhabu iliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Agosti, mwaka huu.

Wabunge hao ni Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima na Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Jerry Silaa ambao walihojiwa na kamati hiyo kwa nyakati tofauti.

Askofu Gwajima na Silaa walikutwa na hatia ya kusema uongo na kudhalilisha muhimuli huo, Azimio la Bunge lilipitisha adhabu ya kutohudhuria mikutano miwili ya Bunge. Gwajima alikutwa na hatia ya kutoa matamshi ya kupinga chanjo ya UVIKO-19.

Silaa alinukuliwa akiongea na wananchi jimboni kwake Julai mwaka 2021, kuhusu masuala ya miamala, kwa kutaka wabunge watozwe kodi kwenye mishahara yao.

Wabunge hao walihojiwa na kamati hiyo chini ya Mwenyekiti Emmanuel Mwakasaka, Agosti 23 na 24, mwaka 2021.

## M/kiti mtaa auawa nje ya nyumba yake

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Mtaa wa Hasanga, Kata ya Uyole jijini Mbeya, Justine Namwinga (47), ameuawa na watu wasiojulikana nje ya nyumba yake baada ya kuchomwa na kitu chenye ncha kali eneo la kifuani majira ya alfajiri jana.

Kwa mujibu wa maelezo ya jirani wa mwenyekiti huyo, Jenita Mahenge alisema tukio hilo limetokea alfajiri ya kuamkia Januari 31 nyumbani kwa Namwinga, ambapo ilidaiwa marehemu alisikika nje akipiga kelele kuita mwizi.

Mahenge alisema yeye na mumewe walitoka nje majira ya saa kumi alfajiri na kumkuta Namwinga jirani na nyumba yao akiwa amelala na baada ya kumuuliza alisema wezi wamekimbia kisha kukata kauli hadi umauti unamkuta.

Alieleza kuwa sehemu aliyolala marehemu waliona kisu kilichokuwa na damu pembeni, begi, runinga hivyo na kufanya mawasiliano na Polisi ambaye aliwajibu hawezi kufika kwa sababu yuko kituoni peke yake na kukubaliana kutafuta gari la kumpeleka hospitali.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Christina Musyani, alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa 04:30 alfajiri baada ya marehemu kuchomwa kisu kifuani chini ya titi la upande wa kushoto.

# HEBRON WA TEMBO WARRIORS AITWA UTURUKI KWA MAJARIBIO

**Na Saada Akida**

BEKI wa timu ya Tanzania kwa Watu wenye Ulemavu, 'Tembo Warriors', Shedrack Hebron, amepata nafasi ya kwenda kufanya majaribio ya kucheza soka la kulipwa katika Klabu ya Yeditepe ya nchini Uturuki.

Kuhitajika kwa beki huyo kumekuja siku chache baada ya mshambuliaji wa Tembo Warriors, Frank Ngailo, kuchukuliwa kwa majaribio na Klabu ya Izmir BBSK ya nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu (TAFF), Peter Sarungi, alisema wamepokea taarifa rasmi kutoka Klabu ya Yeditepe ikimuhitaji Hebron kwa ajili ya majaribio.

**Alisema Yeditepe imefanya mawasiliano hayo kupitia kocha wa klabu hiyo, waki hitaji nyota huyo kwenda kufanya majaribio na akifanikiwa atasajili moja kwa moja kucheza soka la kulipwa.**

"Mazungumzo yanaendelea na uongozi wa klabu inayomhitaji Hebron kwa ajili ya kufanikisha usajili wake kwenda kufanya kwanza majaribio nchini Uturuki, tutaendelea kutoa taarifa zaidi ya mazungumzo yetu," alisema Sarungi.

Alisema wao kama shirikisho wanaona fahari wachezaji wao kupata timu za kucheza nje kwani kutasaidia kuongeza ushindani na kupata uzoefu mkubwa na kuisaidia timu yao ya taifa.

"Nina matarajio makubwa ya wachezaji wetu hao wawili, Hebron anayeenda nchini humo kufanya majaribio na Ngailo ambaye yuko huko kwa sasa, kwani watatusaidia kuelekea katika mashindano ya Kombe la Dunia linalotarajiwa kufanyika mwaka huu nchini humo," alisema Sarungi.

**RUKSA MPYA...**



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akiwasili katika Ofisi za MultiChoice Tanzania mapema jana asubuhi ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake kwa wadau wa sekta ya habari na mawasiliano. Walioambatana naye ni Mwenyekiti na Mmiliki Mkuu wa MultiChoice Tanzania, Balozi Ami Mpungwe (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Jacqueline Woiso. Akiwa MultiChoice, Waziri Nape alitangaza rasmi idhini ya kurushwa kwa chaneli za Tanzania (local Channels) kwenye visimbuzi vyote kuanzia sasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tamasha la tamaduni za Kichina lazinduliwa

**Na Faustine Feliciane**

KITUO cha Utamaduni cha Watu wa China kilichoko chini ya Ubalozi wa China nchini Tanzania, kimezindua Tamasha la Utamaduni la nchi hiyo kikiadhimisha 'Mwaka Mpya wa Kichina'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kituo hicho jijini Dar es Salaam juzi, tamasha la mwaka huu litaadhimishwa kwa njia ya mtandao kutokana na changamoto ya virusi vya corona, hii ikiwa ni mara ya pili kwa tamasha hilo kuadhimishwa kwa njia ya mtandao.

"Tamasha hili la kimataifa linaadhimishwa kwenye balozi zote za China katika nchi mbalimbali na litaonyesha mila na tamaduni mbalimbali za China kwa kucheza ngoma mbalimbali," ilisema sehemu ya taarifa hiyo iliyosainiwa na Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Mingjian.

Alisema tamasha hilo lililozinduliwa wiki iliyopita litaendelea mpaka Februari 15, mwaka huu, litakapofikia mwisho kwa mwaka huu.

"Mambo mbalimbali yatafanyika kwenye tamasha hili kama ngoma na vyakula vya Kichina kwa kuonyeshwa kwenye filamu fupi pamoja na maonyesho ya picha ya 'Auspicious Reunion" na Joyful Celebration", alisema Balozi Mingjian. Tamasha hilo la mwaka huu linaenda pamoja na uzinduzi wa michezo 24 ya Olimpiki inayofanyika mwaka huu nchini China kwenye Jiji la Beijing.

Kwa upande wake Mshauri wa Utamaduni na Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni wa China hapa nchini, Wang Siping, alisema Watanzania kupitia tamasha hili la Spring watapata fursa ya kuona na kufuatilia tamaduni za China.

"Tamasha la Kitamaduni la Kichina limekuwa maarufu zaidi duniani, na linaadhimishwa duniani kote na mwaka huu tunategemea litakuwa la kitofauti zaidi," alisema.

Kwa Tanzania hii ni mara ya pili tamasha hili linafanyika kwa mafanikio zaidi huku Wachina wanaoishi hapa nchini wakipata fursa ya kuungana na wenzao duniani kote kuadhimisha tamasha hilo kubwa.

# *Vivier atoa sababu mechi KMC FC kuwa ngumu*

**Na Saada Akida**

HUKU wakianza safari jana ya kuifuata KMC FC jijini Dar es Salam kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati amesema licha ya kuwa tayari kwa mchezo huo, wanatambua kwamba hautakuwa rahisi kwao.

Biashara United itakuwa ugenini katika mchezo huo utakaopigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Azam Complex, ulioko Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Vivier alisema kikosi chake kipo tayari kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo licha ya kutambua kwamba hautakuwa rahisi kwa pande zote.

Alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu ya kiufundi kufahamiana vizuri, huku akijua mbinu na ufundi wa kocha wa KMC FC, Thierry Hitimana ambaye anamchukulia kama ndugu yake.

"Hii itakuwa mechi ngumu na ushindani mkubwa ukizingatia Hitimana anafahamu uwezo wangu wa kufundisha pamoja na mimi kujua uwezo wake, ninatarajia mechi ngumu," alisema Vivier.

Alisema mbali na kufahamia kiufundi, lakini watakutana na ugumu kwa sababu wapinzani wao wametoka kupoteza katika michuano ya Kombe la Shirikisho hatua ya 32 dhidi ya Ruvu Shooting.

"Tunajiandaa vizuri zaidi nina imani KMC FC watakuja kwa hasira, lakini tumejipanga vizuri kuhakikisha tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Vivier.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND KUONDOKA DORTMUND

MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Braut Halaand mwenye umri wa miaka 21, anataka kuondoka klabu ya Borussia Dortmund katika msimu wa majira ya joto ili kujiunga na Barcelona. (**Express**)

### ALI KUTUA AC MILAN

AC Milan huenda itawasilisha ombi la kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur, Delle Ali mwenye umri wa miaka 25 kwa mkopo. (**Gazzetta dello Sport**)

### HENDERSON KUAMKIA NEWCASTLE

GOLIKIPA wa Manchester United na England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 24, anatarajiwa kutia saini ya mkopo katika klabu ya Newcastle siku ya mwisho katika dirisha la uhamisho. (**Talksport**)

### CALETA-CAR KWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imewasilisha ombi la dau la pauni milioni 18 kumsajili beki wa Marseille na Croatia, Duje Caleta-Car mwenye umri wa miaka 25. (**Goal**)

### DEMBELE KUONDOKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, huenda akaondoka katika klabu hiyo ya Hispania licha ya kuweka makubaliano na PSG, Manchester United imeingia katika kinyang'anyiro cha kumsaini mshambuliaji huyo wa Ufaransa kwa dau la euro milioni 20. (**Journalist Pedro Almeida**)

### SPURS NAO KWA DEMBELE

KLABU ya Tottenham Hotspur pia ina nia ya kumsajili Ousamane Dembele, lakini haiko tayari kulipa mshahara anaotaka. (**Marca**)

### AUBAMEYANG KUBAKI ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, amekubali kuendelea kucheza katika klabu hiyo ili kumaliza kipindi cha msimu uliobakia. (**Sport**)

### NKETIAH AGOMEWA PALACE

OMBI la pili la Crystal Palace la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah limekataliwa, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa England kubakiza miezi sita kwenye mkataba wake. (**Sky Sports**)

### RAPHINHA AWANIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imewasilisha ombi la kutaka kumsaini winga wa Leeds na Brazil, Raphinha, lakini huenda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, atapatikana katika dirisha la uhamisho la msimu wa majira ya joto. (**Daily Mail**)


### ZAKARIA HUYOOO JUVE

KIUNGO wa kati wa Uswisi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 25, anaelekea kujiunga na Juventus baada ya klabu hiyo ya Italia kukubali mkataba na Borussia Monchengladbach. (**Goal**)

### BISSOUMA AWINDWA UNITED

KIUNGO wa kati wa Mali na Brighton, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25, huenda akaondoka pale Aston Villa, huku Tottenham na Manchester United wakiwa na nia ya kumsajili. (**Journalist**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GREENWOOD AKAMATWA KWA TUHUMA ZA UBAKAJI

United yasema haikubaliani na vurugu za aina yoyote na tayari imefahamishwa kuhusu...

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI wa Manchester United, Mason Greenwood, amekamatwa kwa tuhuma za ubakaji na shambulio kufuatia madai kwenye mitandao ya kijamii.

Polisi wa Manchester, walisema walifahamishwa kuhusu "picha na video za mitandao ya kijamii zilizotumwa na mwanamke akiripoti matukio ya unyanyasaji wa kingono".

**Walisema "tunaweza kuthibitisha kuwa mwanamume mwenye umri wa miaka 20, amekamatwa kwa tuhuma za ubakaji na shambulio."**

Anaendelea kuzuiliwa kwa mahojiano na uchunguzi unaendelea.

Man United hapo awali ilisema mchezaji huyo hatarejea kwenye mazoezi au mechi.

Klabu hiyo ilisema "haikubaliani na vurugu za aina yoyote" na imefahamishwa kuhusu madai hayo kwenye mitandao ya kijamii, lakini haitatoa maoni yoyote zaidi hadi "ukweli utakapothibitishwa".

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye aliichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza Machi 2019, alisaini mkataba wa miaka minne Februari 2021.


LIVE IN PLAY | CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 896

MECHI KALI
SWANSEA
VERSUS
LUTON TOWN
1 | 2.41
X | 3.08
2 | 2.94

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RAMOS 'PANCHA' TENA PSG



**PARIS,** Ufaransa

SERGIO Ramos amepata majeraha mengine ikiwa ni wiki mbili tu kabla ya kukutana na klabu yake ya zamani, Real Madrid kwenye hatua ya 16 bora katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mlinzi huyo wa kati atafanyiwa vipimo ndani ya wiki hii na majibu yatatoka baada ya wiki moja kabla ya mchezo huo kujua ukubwa wa majeraha hayo, na kama atakuwa fiti atajumuishwa kwenye kikosi ambacho kitaenda kupambana na Real Madrid.

Ramos alijiunga na PSG kwa uhamisho huru msimu uliopita baada ya mkataba na klabu yake ya awali kumalizika, pia amefanikiwa kuichezea PSG dakika 283 tu hadi sasa huku akifunga bao moja.

Ramos alifunga bao lake la kwanza Jumapili iliyopita kwenye mchezo dhidi ya Reims, awali ilionekana ndio makali yake yameanza kurudi baada ya kusumbuliwa na majeruhi kwa muda mrefu tangu asajiliwe na klabu hiyo, lakini mambo yamebadilika na 'jini' la majeraha bado linamwandama.



# Alba alia kukosolew

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Jordi Alba amewajibu wakosoaji wake baada ya mwanzo mgumu wa mwaka 2022 kwa upande wa kocha Xavi.

Miamba hao wa Katalunya wamejiondoa katika mashindano mawili mwezi huu baada ya kujiondoa katika michuano ya Supercopa ya Hispania nchini Saudi Arabia na Copa del Rey.

Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Alaves wikendi iliyopita kupitia bao la dakika za mwisho la Frenkie de Jong, ulihakikisha pointi tatu.

Hata hivyo, mchezaji wa kimataifa wa Hispania, Alba anaamini wakosoaji wake wanamkosea, kama ilivyokuwa katika misimu iliyopita.

"Nimehisi kutengwa kwa kukosolewa kwa miaka mingi. Hii si mara ya kwanza kunitokea na ninakubali ukosoaji wote, kwani ni sehemu sarakasi ambayo inazalishwa kati mpira wa miguu."

"Ikiwa nitacheza mchezo mzu wakosoaji hawazungumzii suala hi lakini nikicheza kama siku nyingi wananiua. Lakini hii ni kawaida ninakubali."

Licha ya kustahimili msimu mg mu ndani na nje ya uwanja pa Katalunya, uzoefu wa Alba umesa kama nyenzo ya msimu wa 2021/2

Bosi wa zamani Ronald Koem na Xavi, wote wamemwita kar chaguo lao la uhakika katika beki kushoto msimu huu, licha ya ukoso ji huo kutoka nje.

Ameanza mara 23 kwenye mas indano yote kufikia sasa msimu hu idadi hiyo ikiboreshwa na maraf zake wa zamani Gerard Pique na Se gio Busquets, kutoka kwenye kiko cha nje cha Barcelona.

5,686,220

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/02/22 | 18:00 | Hull City vs Preston | 2.55 | 3.25 | 2.80 |
| 02. 05/02/22 | 18:30 | Maritimo vs GD Estoril | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 05/02/22 | 19:00 | St Etienne vs Montpellier | 2.57 | 3.31 | 2.67 |
| 04. 05/02/22 | 20:30 | Swansea vs Blackburn | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 05. 05/02/22 | 21:00 | Pacos Ferreira vs Portimonense | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 06. 05/02/22 | 23:00 | Twente vs Vitesse Arnhem | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 07. 06/02/22 | 16:00 | Valencia vs Real Sociedad | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 08. 06/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Galatasaray | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 06/02/22 | 16:00 | Amorebieta vs Real Oviedo | 2.79 | 3.04 | 2.55 |
| 10. 06/02/22 | 17:00 | Sampdoria vs Sassuolo | 2.81 | 3.56 | 2.36 |
| 11. 06/02/22 | 18:15 | Barcelona vs Atletico Madrid | 2.40 | 3.26 | 2.97 |
| 12. 06/02/22 | 20:00 | Udinese vs Torino | 2.86 | 3.21 | 2.51 |
| 13. 06/02/22 | 20:30 | Betis vs Villarreal | 2.33 | 3.44 | 2.94 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 01/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:10 | 2256 | Japan vs Saudi Arabia | 1.51 | 3.56 | 6.35 |
| 15:00 | 1222 | Sampdoria Youth vs Fiorentina Youth | 1.98 | 3.52 | 3.23 |
| 15:00 | 1407 | Lebanon vs Iraq | 2.59 | 2.83 | 2.78 |
| 15:00 | 3597 | Vietnam vs China | 3.37 | 3.32 | 1.99 |
| 15:00 | 4598 | Empoli Youth vs Genoa Youth | 2.11 | 3.32 | 3.08 |
| 16:00 | 2478 | Swansea U23 vs Millwall U23 | 2.05 | 3.27 | 3.27 |
| 16:00 | 5721 | Coventry U23 vs Hull City U23 | 1.58 | 4.43 | 4.14 |
| 16:45 | 3848 | Persela Lamongan vs Arema | 4.40 | 3.60 | 1.81 |
| 17:00 | 1879 | Syrian Arab Republic vs South Korea | 5.59 | 3.42 | 1.59 |
| 17:00 | 2890 | AC Milan Youth vs Inter Youth | 2.66 | 3.43 | 2.32 |
| 17:00 | 5005 | FC Goa vs Delhi Dynamos FC | 2.02 | 3.56 | 3.08 |
| 17:30 | 1832 | Iran vs United Arab Emirates | 1.60 | 3.52 | 5.21 |
| 18:00 | 1098 | Omonia Nicosia vs PO Xylotymbou | 1.02 | 10.63 | 33.82 |
| 18:00 | 4345 | AL Nahdha vs Al Khaleej Club | 3.47 | 3.08 | 2.05 |
| 19:00 | 2043 | Oman vs Australia | 5.98 | 3.67 | 1.51 |
| 21:00 | 1161 | Valenciennes vs Nancy | 2.46 | 3.05 | 2.90 |
| 21:00 | 1870 | AJ Auxerre vs Paris FC | 2.16 | 3.19 | 3.29 |
| 21:00 | 2032 | Vere United FC vs Mount Pleasant FC | 4.82 | 3.42 | 1.67 |
| 21:00 | 2580 | Niort vs Dunkerque | 1.86 | 3.34 | 4.13 |
| 21:00 | 2682 | PAU FC vs Nimes | 2.06 | 3.24 | 3.49 |
| 22:45 | 1022 | Dundee FC vs Dundee Utd | 2.36 | 3.20 | 2.95 |
| 22:45 | 1429 | Salford City vs Carlisle | 1.88 | 3.40 | 3.94 |
| 22:45 | 2434 | Colchester vs Rochdale | 2.84 | 3.18 | 2.42 |
| 22:45 | 3106 | St Mirren vs Motherwell | 2.33 | 3.15 | 3.05 |
| 22:45 | 3234 | Tranmere vs Stevenage | 2.01 | 3.34 | 3.54 |
| 22:45 | 3511 | Port Vale vs Forest Green | 3.44 | 3.39 | 2.02 |
| 22:45 | 3796 | Partick Thisle vs Ayr United | 1.74 | 3.52 | 4.40 |
| 22:45 | 3893 | Hibernian vs Hearts | 2.45 | 3.16 | 2.86 |
| 22:45 | 4111 | Swansea vs Luton Town | 2.41 | 3.08 | 2.94 |
| 22:45 | 4151 | Southend vs Barnet | 2.19 | 3.42 | 2.98 |
| 22:45 | 4176 | Doncaster vs Rotherham | 7.66 | 4.61 | 1.36 |
| 22:45 | 4301 | Gillingham vs Crewe | 2.41 | 3.19 | 2.84 |
| 22:45 | 4303 | Northampton vs Barrow | 1.87 | 3.44 | 3.93 |
| 22:45 | 4323 | Ross County vs Aberdeen | 3.06 | 3.11 | 2.34 |
| 22:45 | 4633 | AFC Wimbledon vs Cheltenham | 2.24 | 3.24 | 3.09 |
| 22:45 | 4868 | Swindon Town vs Crawley Town | 1.89 | 3.48 | 3.78 |
| 22:45 | 4976 | Bradford City vs Leyton Orient | 2.29 | 3.18 | 3.04 |
| 22:45 | 5018 | Sheffield Wed vs Morecambe | 1.47 | 4.32 | 5.89 |
| 22:45 | 5043 | Harrogate vs Mansfield | 2.60 | 3.29 | 2.55 |
| 22:45 | 5175 | Millwall vs Preston | 2.22 | 3.13 | 3.23 |
| 22:45 | 5334 | Livingston vs St Johnstone | 2.25 | 3.06 | 3.30 |
| 22:45 | 5496 | Wigan vs Oxford Utd | 2.02 | 3.39 | 3.44 |
| 22:45 | 5689 | Yeovil vs Weymouth | 1.63 | 3.93 | 4.61 |
| 22:45 | 5865 | Raith Rovers vs Queen of South | 1.73 | 3.66 | 4.29 |
| 23:00 | 1960 | Bolton vs Cambridge Utd | 1.84 | 3.54 | 3.94 |
| 23:00 | 2471 | Bolivia vs Chile | 2.60 | 3.20 | 2.75 |
| 23:00 | 5625 | Aberystwyth Town vs Haverfordwest | 2.28 | 3.37 | 2.74 |
| 23:15 | 5446 | Santa Clara vs Boavista | 2.22 | 3.11 | 3.30 |
| 23:15 | 5793 | Arnett Gardens FC vs Humble Lions FC | 1.66 | 3.43 | 4.83 |
| 23:30 | 2431 | Real Cartagena vs Fortaleza (COL) | 2.66 | 3.14 | 2.47 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# GEITA GOLD YAFUNGUKA KUPATA MCHEKEA FA

**Na Adam Fungamwango**



TIMU ya Geita Gold ambayo itacheza dhidi ya Mbuni FC kwenye mechi ya 16-bora ya Kombe la FA, imesema lengo lao ni kucheza hatua ya fainali ya michuano hiyo, huku ikidai kucheza na timu zinazodaiwa kuwa ni mchekea wao sio wanaopanga ratiba.

Nahodha msaidizi wa timu hiyo, Pius Luchagula, alisema hayo, baada ya timu hiyo juzi, kuitwanga Tunduru Korosho mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyankumbu na kutinga hatua ya 16-bora ya michuano hiyo.

"Mechi haikuwa rahisi kama mashabiki wetu walivyodhani, eti kwa sababu timu ipo daraja la pili, ndiyo maana tumepata ushindi wa mabao 2-0, lakini lengo ilikuwa tufuzu," alisema mchezaji huyo.

Kuhusu kutoka kucheza dhidi ya Tunduru Korosho na sasa kuelekea kucheza dhidi ya Mbuni FC, Luchagula alisema kuwa wao wanachojua ni kucheza soka, na wala hawaangalii wanacheza na nani, hivyo kuonekana wanapangwa na timu mchekea kwenye michuano hiyo si kazi yao.

"Sisi hatupangi ratiba, kucheza na Tunduru Korosho na baadaye Mbuni FC siyo tatizo, kwa sababu hata kama tukiitoa Mbuni FC tutakutana na timu za Ligi Kuu hatua ya nane bora kwa sababu nina uhakika zitakuwa zimebaki, na sisi wote lengo la klabu ni kufika hatua ya fainali. Unajua ukifika fainali unakuwa na uwezekano wa kucheza mechi za kimataifa," alisema.

Mbuni FC inakutana na Geita Gold baada ya kuiondoa Lipuli FC kwenye michuano hiyo kwa mikwaju ya penalti 4-3, kutokana na dakika 90 za mchezo kumalizika kwa sare tasa.

# *Tango kidedea Waitara Trophy*




**Na Saada Akida**

MCHEZAJI wa gofu, Mhandisi Joseph Tango, ameibuka kidedea na kutangazwa mshindi wa jumla kwa Mikwaju 68, katika Shindano la Waitara Trophy, lililofanyia katika viwanja vya Klabu ya Lugalo, Dar es Salaam juzi.

Katika shindano hilo maalumu kwa ajili ya kutambua mchango wa Mkuu wa Majeshi mstaafu, Jenerali George Waitara, kwenye mchezo wa gofu, ambaye ni mwazilishi wa Klabu ya Lugalo, washindi wengine kwa wachezaji wa kulipwa ni Frank Mwinuka kwa mikwaju 70, Fadhili Nkya (mikwaju 73) na Abdallah Yusufu (mikwaju 75).

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi, mgeni rasmi katika shindano hilo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema katika jitihada za kutangaza vivutio vya utalii nchini serikali imeongeze mchezo wa gofu.

Naye Jenerali Waitara, alisema njia pekee ya kukuza gofu ni kuwekeza kwenye viwanja katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kuwa na viwanja katika maeneo mbalimbali nchini na jitihada zinafanyika kuongeza kiwanja cha gofu katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, kwa ajili ya ushawishi wa watalii na kuendeleza kukuza mchezo huu wa gofu," alisema Jenerali Waitara.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Brigedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo, alisema Shindano la Waitara Trophy limeanzishwa kwa ajili ya kumbukumbu ya klabu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

# Michezo

Jumanne Februari 1, 2022

Nipashe





## Greenwood akamatwa kwa tuhuma za ubakaji


UKURASA 21

NUSU DAZENI...



Mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu, akiifungia timu yake bao la sita wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Dar City kwenye mechi ya Kombe la FA hatua ya 32 - bora iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: SIMBA**


## Ramos apata 'pancha' tena PSG




**PARIS,** Ufaransa

SERGIO Ramos amepata majeraha mengine ikiwa ni wiki mbili tu kabla ya kukutana na klabu yake...

HABARI UK. 22




## Alba alia kukosolewa Barcelona

**BARCA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Jordi Alba amewajibu wakosoaji wake baada ya mwanzo mgumu wa mwaka 2022 kwa upande wa...

HABARI UK. 22

# SIMBA SASA MGUU SAWA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## ●●● Wachezaji wasema sasa mwendo wa mabao tu, Matola atoa siri ya ushindi...

USHINDI wa mabao 6-0 iliyoupata Simba kwenye mechi ya Kombe la FA hatua ya 32- bora dhidi ya Dar City juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, umewafungua 'mdomo' baada ya uongozi wa klabu hiyo kusema ulikuwa ni kama wakujiweka sawa kuelekea mechi zijazo.

**Kabla ya kuibuka na ushindi huo mkubwa juzi, Simba ilicheza mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu bila kupata ushindi ikipoteza mbili kwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City na Kagera Sugar na kutoka suluhu dhidi ya Mtibwa Sugar, hivyo ikishindwa kufunga hata goli moja.**

Simba ambayo sasa itacheza dhidi ya Ruvu Shooting hatua ya 16-bora, Februari 15, kabla ya mchezo huo inakabiliwa na mechi mbili; moja ya Ligi Kuu Jumapili wiki hii dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kisha Februari 13, mwaka huu, itaikaribisha Asec Mimosas ya Ivory Coast kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema ushindi mkubwa walioupata ulikuwa ni kama kujiweka sawa kwa mechi zinazofuata.

"Hii ndiyo Simba ambayo mashabiki wanataka kuiona, watu wamepata furaha, tumeonyesha kuwa sisi tuna kikosi bora na chenye thamani. Shida kubwa iliyokuwa inatukabili ni ya ufungaji, lakini leo umeona tumepata mabao mengi, sasa tunarudi kwenye ligi, tuna mechi mbili na timu za Prisons, halafu Mbeya Kwanza kabla ya kwenda kwenye michuano ya kimataifa," alisema Ahmed.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Simba, Suleiman Matola, ambaye alikiongoza kikosi hicho kuibuka na ushindi huo kutokana na Kocha Mkuu, Pablo Franco, kuwa nje ya dimba akitumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu kwa utovu wa nidhamu aliouonyesha kwenye michezo ya Ligi Kuu, kwanza aliwapongeza wachezaji kwa kufuata maelekezo kutoka benchi la ufundi na kusababisha kupatikana kwa ushindi mnono.

Matola alisema walipanga kuanza kwa kasi kwa kuwakabia juu, mbinu ambayo ilifanikiwa na kuweza kupata mabao matatu ndani ya dakika 20 za kwanza.

"Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza wachezaji kwa jinsi walivyojituma muda wote, tulihitaji ushindi huu na tunamshukuru Mungu, tumefanikiwa," alisema Matola na kuongeza.

"Tulipanga kukabia juu na kuanzisha mashambulizi, tulifanikiwa kama umeona ndani ya dakika 20 za mwanzo tukawa tumepata mabao matatu na bado naendelea kuwapongeza wachezaji.

"Huu ulikuwa mchezo muhimu zaidi kwetu, tulihitaji zaidi ushindi ili kurudisha morali yetu baada ya kupitia katika kipindi kigumu kitu ambacho tumefanikiwa hivi sasa tunaangalia michezo ijayo," alisema Matola.

Naye kiungo mshambuliaji wa Simba, Hassan Dilunga, amewaomba mashabiki kuendelea kujitokeza kwa wingi uwanjani kusapoti timu yao huku kwa upande wao wakiahidi kuwapa furaha.

"Nimefurahi kuwapo katika kikosi kilichopata ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Dar City na ninaamini tutaendelea kushinda mechi zijazo," alisema Dilunga.

Wakati Simba wakieleza hayo, Kocha wa Dar City, Almas Shaban, alisema ulikuwa mchezo mgumu kwao kwani walijua wanaenda kukutana na timu kubwa, na walifanya maandalizi mazuri lakini makosa madogo madogo na uzoefu ndiyo yaliyowahukumu ila sasa wamejifunza kitu baada ya kipigo hicho kutoka kwa bingwa mtetezi.

"Tulitengeneza nafasi kadhaa ambazo kama tungekuwa makini huenda tungeweza kupata bao, matokeo haya ni mapungufu ya kikosi changu ambayo naenda kuyafanyia kazi tukijipanga kwa ajili ya michezo ya 'First League' (Ligi Daraja la Kwanza)," alisema kocha huyo.

Mabao ya Simba katika mchezo huo yalifungwa na Meddie Kagere (mawili), Clatous Chama, Rally Bwalya, Pascal Wawa na Chris Mugalu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >